# Siku Hiyo Pale Kalvari

Jeffersonville, Indiana, USA

Septemba 25, 1960

1 Asante, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Ubarikiwe, ndugu!" — Mh.] Mungu akubariki, Ndugu Neville. Asanteni, sana.

Habari za asubuhi, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa maskanini tena, asubuhi ya leo, kumtumikia Bwana, katika njia ya kuhubiri Neno na kuwaombea wagonjwa. Nami ninashukuru sana kwa ajili ya siku hii.

Nami nilishangaa, nilipoingia tu. Ndugu fulani alikuja na kusema, "Sitaki kuwa kama yule mwenye ukoma asiyestahili ambaye aliyeponywa." Ni Ndugu Wright. Nilimwombea, na Bwana amemponya kabisa. Naye akaja, akilia, kunipa mkono, na kusema ya kwamba—ya kwamba angetaka kumshukuru Bwana kwa—kwa kuponywa. Alitaka kurudi na kutoa shukrani. Yote yamekwisha. Yeye—yeye ni mzima kabisa sasa. Tunashukuru kwa ajili ya shuhuda hizo.

2 Na Charlie, wewe na Ndugu Jeffries, mkitaka, njoni hapa na kuchukua viti hivi hapa. Nanyi mmekaribishwa na zaidi ya kukaribishwa, kwa hiyo haitawabidi kusimama. Yule ndugu mwingine pale, na Ndugu Wood, waje tu hapa. Wewe ni … Hapa kuna sehemu chache, chache hapa kwenye benchi, kwa hiyo haitakubidi kusimama. Ninaamini, sehemu kadhaa hapa, na, naam, ungeweza kukaribishwa na zaidi ya kukaribishwa kuja na kuchukua mahali hapa.

Tunafurahi ku … Ninaamini ilisemwa, wakati mmoja, "Nilifurahi waliponiambia …" Mungu akubariki, ndugu. [Ndugu fulani anasema, "Daima napenda kuwa karibu na mhubiri." — Mh.] Asante. Asante, asante. "Nilifurahi waliponiambia, twende nyumbani mwa Bwana." Hiyo ni haki na furaha ya Mkristo, kwenda nyumbani mwa Bwana.

3 Nikiangalia kila mahali, nikiwaona marafiki zangu wengi humu, asubuhi ya leo, nimefurahi sana kwa jambo hili. Nina furaha kuwaona Ndugu na Dada Dauch hapa, kutoka Ohio. Ninamwona Ndugu na Dada Armstrong kule nyuma, kote kutoka Ohio. Mungu awabariki nyote, pia. Na, loo, ukiangalia tu kila mahali, unaona wengi sana, ingekuwa vigumu kupata majina yao wote. Dada Hoover, tuna furaha kukuona, asubuhi ya leo, kutoka huko Kentucky. Na Charlie na Nellie, Ndugu Jeffries na familia yake, na kadha wa kadha, kutoka nje ya mji.

Kwa hiyo tunatarajia wakati mkuu katika Bwana, asubuhi ya leo, tukimtarajia Mungu kukutana nasi kwa njia ya kubariki nafsi zetu na kutuhudumia mambo tunayohitaji.

Na ninapotazama mahali hapa, kama nikienda kuwaita marafiki wangu wote hapa, nitachukua karibu asubuhi, nikisema mambo mbalimbali. Inanifanya nijisikie vizuri kurudi kanisani, kuwaona watu wote ndani, kukutana.

4 Itakuwaje tutakapofika Mbinguni, nasi tutakutana Kule kwa ajili ya ule wakati mkuu wa ushirika wa Milele, wa milele pamoja, kukikalia Kiti cha Enzi cha Mungu, na baraka zile zile ambazo sote tumezithamini? Huko sisi tutafanywa katika sura Yake, katika mfano Wake, na Roho Wake akiwa juu yetu tukimwabudu na kumtumikia Yeye milele yote, hatutachoka kamwe.

Waza tu, hakuna cho chote unachoweza kuwazia, ambacho ungetaka kufanya, ila kile ambacho mara kwa mara kinakuchosha kukifanya. Charlie, nakisia mimi na wewe tumewinda kindi kuliko cho chote ambacho tunapenda kufanya katika njia hiyo, bali mnajua unachoka kufanya hivyo.

Napenda kutembea kwa miguu, kupanda milima na kutembea tu. Bali wakati mwingine mimi huchoka na kutaka kufanya jambo jingine.

Nami ninapenda kuendesha gari. Wakati mwingine mimi huanza kusikia uchovu, kuchoka kabisa na kushikwa na wasiwasi mwingi. Nitaruka tu niingie kwenye gari langu na kuendesha, na kushikilia usukani, nikishuka kwenda barabarani, nikiimba, "Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao," ama kitu fulani. Nikishika sana huo usukani na kuimba na kufanya vishindo kwa mguu wangu na kupiga kelele. Na, vema, baada ya kitambo kidogo, ninachoka, halafu ninarudi nyumbani na kuanza kitu kingine.

Lakini tutakapomwabudu Mungu katika Ufalme huo mpya, hakutakuwako na wakati wa uchovu, tu—daima kutakuwa na baraka, na kuendelea daima. Lakini, bila shaka, tutakuwa tumebadilishwa wakati huo. Hatutakuwa kama tulivyo sasa. Tungekuwa viumbe mbalimbali, tofauti na tulivyo wakati huu. Kwa hiyo, tuna furaha.

5 Nilikuwa nikiwazia tu. Sijui kama niliwahi kufanya hivyo, nilinukuu hili au la. Ndugu Charlie, wakati fulani uliopita, nilikuwa huko chini Kentucky pamoja naye, naye akasema, "Ndugu Branham, unafikiri, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, mimi na wewe tutawinda kindi?"

Nikasema, "Sidhani hivyo, Charlie."

Akasema, "Vema, tunapenda sana kufanya hivyo, u—unafikiri tutafanya hivyo tutakapoingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu?"

Nikasema, "La, hakuna kitu kitakachouawa katika ule Utawala wa Miaka Elfu."

Naye akasema, "Vema, tunapenda sana jambo hili."

Nikasema, "Charlie, vipi kama ningeweza kukusadikisha kwamba wakati mmoja ulikuwa ni nguruwe pori, nawe ulikuwa umefufuka ukawa wa hali ya juu, ukawa mwanadamu? Je, ungelitaka kamwe kurudi nyuma ukafurahie anasa za nguruwe mwitu?"

Kasema, "La."

Nikasema, "Waona, ungelikuwa juu sana kuliko nguruwe mwitu sasa kwa kuwa wewe ni mwanadamu, haungalitaka kuwa nguruwe mwitu tena." Nikasema, "Sasa zidisha hilo kwa elfu kumi, na hivyo ndivyo utakavyokuwa wakati utakapobadilishwa kutoka hapa kuwa kile utakachokuwa. Hutataka kuwa mwanadamu tena."

Hiyo ni kweli. Itakuwa ni kitu tofauti. Nina furaha sana kwa ajili ya mawazo yake, nikijua ya kwamba siku moja tutapanda juu zaidi.

6 Vema, sasa, kama Bwana akipenda, Jumapili ijayo, ambayo itakuwa karibu … Ndipo nitaondoka, kwenda huko Wyoming, pamoja na rafiki mzuri; ama huko nje Idaho, pamoja na rafiki yangu mzuri, Ndugu Miner Arganbright, Ndugu Clayt Sonmore, Wafanyi Biashara Wakristo.

Juma lijalo, juma baada ya lingine, ni sasa; wa 7, nitakuwa huko—huko Dallas, Texas, kwenye Mkutano wa Sauti ya Uponyaji. Na nitahubiri katika usiku wa tarehe saba. Na halafu ninarudi, kwenda huko Idaho pamoja na Ndugu Arganbright na Wafanyi Biashara Wakristo. Na labda tutakuwa na usiku mmoja huko Minneapolis, kabla hatujaondoka. Kisha mara moja katika kifungua kinywa cha Wafanyi Biashara Wakristo.

Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi nataka kurudi humu Maskanini tena, na kama hiyo inaruhusiwa na iwe ni mapenzi ya Bwana. Nami ninataka kuzungumza juu ya somo la *Upepo wa kisulisuli Katika Upepo*, kama Bwana akipenda. Ilionekana kuwa moyoni mwangu, juma zima.

7 Na hivi majuzi asubuhi, asubuhi na mapema yapata saa 10 usiku, niliamka nikapata wazo hili *Siku Hiyo Pale Kalvari*. Nami nataka kuzungumza juu ya jambo hilo, asubuhi ya leo: *Siku Hiyo Ya Kalvari.*

Na sasa kwa kusoma huku, hebu na tufungue sasa katika Biblia zetu, katika Maandiko, kwenye Injili ya Mathayo Mtakatifu, kwenye mlango wa 27. Nasi tutaanza na kifungu cha 27 na kusoma sehemu ya Maandiko haya, tupate msingi wetu, ndipo tutaanza mara moja. Na baada ya ibada ya kuhubiri, basi tutawaombea wagonjwa.

8 Tangu mara ya mwisho hapa, nikikumbuka, kwa kulinganisha huduma yangu mpya. Nilipata shuhuda nyingi zaidi kutoka katika mkutano huo kuliko nilizopata katika mkutano wo wote kwa muda mrefu.

Kuna jambo ambalo kwamba huna budi kuwasiliana na mtu mwenyewe haidhuru ni mambo mangapi ya kimbinguni yanayoonyeshwa. Lakini mnaona, uponyaji hauna budi kutegemea imani ya mtu binafsi. Sasa, kama mtu binafsi ana imani …

Nao waone endapo Roho Mtakatifu anaenda juu ya wasikilizaji na kusema, "mambo fulani na fulani yatatendeka. Jina lako ni *fulani*. Na umetoka mahali fulani. Na jambo *fulani* ulilotenda. Na itakuwa *hivi*." Na kuona yote hayo yakitukia hivyo tu!

Hata hivyo, mtu huyo, anayeketi hapo, anapaswa kutazama juu na kusema, "Hapana shaka huyo ni Mungu. Ninakubali uponyaji wangu."

Lakini, badala ya jambo hilo, mtu binafsi anasema, "Niwekee mikono na uniombee, ili nipate kuponywa." Lakini hivyo ndivyo tulivyofundishwa hapa Amerika na, kwa hiyo, tuamini hivyo. Na hilo hakika ni la Kimaandiko.

9 Bali sasa tunaona, kule Afrika na mahali mbalimbali, hebu tu jambo kama hilo litendeke, wasikilizaji wote wanainuka mara, moja na kuukubali uponyaji wao, kwa sababu hawajafundishwa lo lote. Mnaona? Hata hawajafundishwa uponyaji. Na halafu wanapoona jambo hilo, wanajua ya kwamba kuna Mungu aliye hai. "Na kama Yeye yu hai, Yeye—Yeye ni mkuu, na Yeye—Yeye huponya." Na hivyo ndivyo ilivyo, kwa sababu msingi tayari umewekwa, misingi, ya kwamba Yeye ni mponya, na huwaponya watu. Ndipo wanapoona Uwepo Wake ukitenda kazi kupitia Kanisa Lake, ndipo wanasema, "Hilo latosha. Hilo tu ndilo tunalohitaji."

Lakini sisi tumefundishwa, "kuwawekelea wagonjwa mikono," na mambo kama hayo. Hiyo ndiyo sababu haitendi kazi vizuri sana katika Amerika.

Sasa, kumbukeni, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda, Ndugu Neville atalitangaza, bila shaka. Na ni *Upepo wa Kisulisuli Katika Upepo*.

10 Sasa, nilikuwa nikiwapa muda mchache kufungua Maandiko yenu, kwenye Mathayo 27. Hebu tuanze kusoma kwenye—kwenye kifungu cha 27, cha Injili ya Mathayo Mtakatifu. Sasa hebu tusikize kwa makini tunaposoma.

> *Nao askari wa liwali wakamchukua Yesu ndani ya Praitorio, wakamkusanyikia kikosi kizima.*
>
> *Wakamvua nguo, wakamvika vazi jekundu.*
>
> *Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake: wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, Salamu, Mfalme wa Wayahudi!*
>
> *Kisha wakamtemea mate, wakautwaa ule mwanzi, wakampiga-piga kichwani.*
>
> *... Walipokwisha kumdhihaki, wakalivua lile vazi, wakamvika mavazi yake, wakamchukua kumsulubisha.*
>
> *Hata walipokuwa wakitoka, wakamwona mtu Mkirene, jina lake Simoni; huyu wakamshurutisha auchukue msalaba wake.*
>
> *Na walipokwisha kupanda kwenda…walipokwenda mahali paitwapo Golgotha, yaani, Fuvu la kichwa,*
>
> *Wakampa kunywa divai iliyochanganyika na nyongo; ... lakini yeye alipoionja hakutaka kuinywa.*
>
> *Walipokwisha kumsulubisha, waligawa mavazi yake, wakapiga kura; Lili litimie neno lililonenwa na nabii, Waligawa nguo zangu kati yao, na juu ya vazi langu walipiga kura.*
>
> *... wakaketi, wakamlinda huko.*
>
> *Wakaweka ... juu ya kichwa chake mashtaka yake, yaliyoandikwa HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI.*
>
> *Wakati uo huo wanyang'anyi wawili wakasulubiwa pamoja naye, mmoja mkono wake wa kuume, na mmoja mkono wake wa kushoto.*
>
> *Nao—nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa-tikisa vichwa vyao, wakisema,*
>
> *Ewe uliyelivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe nafsi yako; ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani.*
>
> *Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi na wazee, wakasema,*
>
> *Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Kama yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini.*
>
> *Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama atamwokoa; kwa maana alisema, Mimi ni Mwana wa Mungu.*
>
> *Pia wale wanyang'anyi waliosulubiwa pamoja naye, walimshutumu vile vile.*
>
> *Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa.*
>
> *Kama saa tisa, Yesu akapasa sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*
>
> *Na baadhi ya waliohudhuria, waliposikia, walisema, Huyu anamwita Eliya.*
>
> *Mara mmoja ... akaenda mbio, akatwaa sifongo, akaijaza siki, akaitia juu ya mwanzi, akamnywesha.*
>
> *Wale wengine wakasema, Acha; na tuone kama Eliya atakuja amwokoe.*
>
> *Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho yake.*
>
> *Tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka;*

*na miamba ikapasuka;*

*... Makaburi yakafunuka; ikainuka miili mingi ya Watakatifu waliolala,*

*Nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake, wakauingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi.*

*Basi yule akida, na hao waliokuwa pamoja naye wakimlinda Yesu, walipoliona tetemeko la nchi na mambo yaliyofanyika, wakaogopa sana, wakisema, Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu."*

11 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

Bwana, tunajua ya kwamba Wewe ni Mungu. Nayo … Baada ya kusoma Neno hili takatifu lililowekwa wakfu, bado tunaweza kuona ya kwamba asili Yako haijabadilika. Wewe daima ni Mungu. Na ilionekana kana kwamba Yesu asingalipata msaada wo wote, ya kwamba Yeye alichukuliwa na mikono miovu na kukatakatwa vipande, akatemewa mate, akadhihakiwa na huku amesulubishwa msalabani, akitokwa na damu, akifa. Na ilionekana kana kwamba hakukuwa na msaada, mahali po pote, mpaka hata Yeye akalia, Mwenyewe, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?"

Lakini, Wewe unatenda katika wakati ambapo hakuna kitu kingine chochote kinachoweza kutenda kazi. Tumepewa kujua, Bwana, ya kwamba kama tuna mito yoyote ambayo hatuwezi kuvuka, kama tuna milima tusiyoweza kupanda, Mungu ni stadi wa kutenda mambo ambayo wengine hawawezi kufanya.

Wewe ni stadi, wa kazi hiyo, kwa kuwa Wewe unajua sababu ya siku hiyo pale Kalvari. Wewe, ukiwa ni Mungu, Yeye asiye na kikomo, ulijua wakati huu hauna budi kuja. Lakini ulipotimizwa, basi ulionyesha ya kwamba Wewe ulikuwa Mungu. Ulionesha ni Nani aliyekuwa bosi. Uliitikisa nchi, na watakatifu waliolala ardhini wakafufuka. Ulilitia giza jua usiku, kama giza la usiku, ikionesha ya kwamba Wewe ulikuwa Mungu. Lakini Wewe ulionekana kuwa kimya kwa muda mrefu.

12 Hebu na sisi, kutokana na jambo hili, tufikie hitimisho hili, ya kwamba, mradi tu tunatembea katika Roho, tukiongozwa na mkono wa Mungu, haidhuru kile kinachoonekana ni kosa, hata hivyo tunaelekea Kalvari; Mungu atanena katika saa inayofaa, katika wakati unaofaa.

Sasa, Baba Mungu, tungeomba msamaha wa dhambi zetu na makosa yetu. Tungeomba Roho Wako atuongoze. Tuongoze, kama vile Hua alivyomwongoza Mwana-Kondoo. Hebu na tuwe watiifu kwa cho chote kinachotupata, tukijua jambo hili, ya kwamba Mungu hutenda mambo yote vizuri, na kujua ya kwamba itakuwa sawa.

Uwe pamoja nasi leo katika ibada hii. Tunaomba ya kwamba utawaokoa wale walio katika hali ya kuokolewa, na wanaotafuta wokovu. Wajaze hao na uzima wa milele, ambao wanaoutafuta. Tunaomba ya kwamba utawaponya wale walio wagonjwa na wanaoteseka, ambao wamekuja, wakitafuta uponyaji. Nasi tutakusifu kwa ajili ya jambo hilo. Tunaomba katika Jina la Mwanao, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

13 Sasa, katika kunena asubuhi ya leo, tunataka kuvuta usikivu wenu kwa somo nililochagua kuzungumza kutoka: *Siku Hiyo Pale Kalvari.*

Inaonekana kana kwamba ingekuwa nje kidogo ya msimu wake; hii inapaswa iwe kwenye Ijumaa Kuu. Kalvari inapaswa kukumbukwa kila siku. Nasi tumesikia mengi sana juu yake, tumesoma mengi sana juu yake. Wahubiri wamehubiri juu yake, tangu mwanzo wa wakati. Waimbaji wameimba juu yake, katika nyakati zote. Manabii walitabiri jambo hilo, miaka elfu nne kabla halijatukia. Nao manabii wa siku hizi wanaelekeza nyuma wakati ilipotendeka. Ni siku muhimu sana! Ni moja ya siku muhimu sana katika siku zote ambazo Mungu aliwahi kupambazuka duniani.

14 Na kama ni muhimu sana kwa jamii ya binadamu, Kalvari, nafikiri ni vema kwetu kurudi nyuma na kulichunguza, na tuone maana yake kwetu. Kwa maana, nina hakika, katika saa hii ya mwisho tunayoishi, tunatafuta kila umuhimu wa Mungu ambao tunaweza kujua. Na yote tuwezayo kujua, tuko hapa kujifunza habari zake, kuona yale yaliyo kwa ajili yetu, na yale ambayo Mungu ametufanyia, na kuona yale Yeye ameahidi kutufanyia. Na hiyo ndiyo sababu ya sisi kuja kanisani. Hiyo ndiyo sababu mhubiri huhubiri, hiyo ndiyo sababu anajifunza na kutafakari Maandiko, na kutafuta uvuvio, ni kwa sababu yeye ni mtumishi wa umma kwa watu wa Mungu. Naye anajaribu kupata kitu ambacho kitaninii … ambacho Mungu angepaswa kuwaambia watu Wake, kitu ambacho kingewasaidia. Labda, huenda ikawa, kuwahukumu katika dhambi zao, bali ingekuwa msaada wa kuwainua, kusudi wapate kuziacha dhambi zao kisha wainuke ili wamtumikie Bwana. Na wahudumu wanapaswa kutafuta mambo haya.

15 Iwapo siku hii ni muhimu sana, moja ya siku zilizo kuu sana, hebu na tuangalie mambo matatu ambayo siku hiyo ilimaanisha kwetu. Tungeweza kuchukua mamia. Lakini, asubuhi ya leo, nimechagua tu mambo matatu mbalimbali, muhimu tunayotaka kuangalia, kwa dakika chache zijazo, ambayo Kalvari

ilimaanisha kwetu. Nami naomba ya kwamba itamhukumu kila mwenye dhambi aliyeko, ya kwamba itamfanya kila mtakatifu kupiga magoti yake, ya kwamba itamfanya kila mgonjwa ainue imani yake kwa Mungu na aondoke ameponywa, kila mwenye dhambi aokolewe, kila aliyerudi nyuma arudi na ajionee aibu, na kila mtakatifu afurahi na apate kitu kipya cha kushikilia na tumaini jipya.

16 Jambo moja kuu muhimu ambalo Kalvari inamaanisha kwetu na ulimwengu ni, ilimaliza swali la dhambi mara moja tu. Mwanadamu alipatikana na hatia ya dhambi. Na dhambi ilikuwa ni adhabu ambayo hakuna mtu angeweza kulipa. Adhabu ilikuwa kubwa sana hata hapakuwapo na mtu ye yote ambaye angeweza kulipa adhabu hiyo. Kwa kweli ninaamini ya kwamba Mungu alilikusudia namna hiyo, ya kwamba adhabu ingekuwa kubwa sana hivi kwamba hakuna mtu angaliweza kuilipa, ili aweze kuifanya, Mwenyewe. Sasa, adhabu ya dhambi ilikuwa mauti. Nasi sote tulizaliwa katika dhambi, tukaumbwa katika uovu, tukaja ulimwenguni, tukisema uongo. Kwa hiyo hapakuwapo na mmoja wetu aliyestahili, ama, wasingeweza kumpata mtu yeyote duniani aliyestahili.

17 Na dhambi haikuanza duniani. Dhambi ilianza Mbinguni. Lusifa alikuwa … Lusifa, Ibilisi, alikuwa kiumbe kilichohukumiwa, kwa sababu ya kutotii kwake, kabla hajaipiga dunia. Dhambi ilianza Mbinguni, ambapo Mungu aliwaweka Malaika, na kadhalika, juu ya msingi ule ule aliowaweka wanadamu; maarifa, mti wa maarifa, mti wa Uzima na mti wa maarifa, ambapo mwanadamu angeweza kuchukua chaguo lake. Na Lusifa alipopewa mamlaka ya kuchagua, yeye alitaka kitu bora kuliko kile alichokuwa nacho Mungu. Hilo lilisababisha shida.

18 Na kulikuweko na deni la dhambi. Madai yake yalikuwa mauti. Adhabu ilikuwa mauti. Na, hiyo ni, tungeweza kuzungumzia hili kinaganaga, kwa maana siamini kuna mauti ila moja. Kuna Uzima mmoja. Ninaamini mtu aliye na Uzima wa Milele hawezi kamwe kufa. Nami ninaamini kuna kuangamizwa kabisa kwa mtu huyo anayetenda dhambi, kwa kuwa Biblia ilisema, "Nafsi itendayo dhambi, hakika itakufa." Si mtu huyo; "*Nafsi* itendayo dhambi." Kwa hiyo, hakika Shetani hana budi kufa, apate kuangamizwa kabisa. Jinsi ambavyo sikubaliani na walimwengu wote wanaosema ya kwamba Shetani ataokolewa! Alitenda dhambi, naye ndiye mwanzilishi wa dhambi. Na nafsi yake ilitenda dhambi; Naye alikuwa ni roho. Roho hiyo itaangamizwa kabisa, kusiwepo kitu cho chote kilichosalia.

19 Nayo dhambi ilipoingia duniani kule nyuma mwanzoni kama shuka nyeusi ikishuka kutoka mbinguni, ilipoozesha dunia. Ilikitupilia kila kiumbe duniani, na viumbe vyote vya Mungu, utumwani. Mwanadamu alikuwa chini ya utumwa wa mauti, magonjwa, shida, huzuni. Viumbe vyote vikaanguka pamoja naye. Dhambi ndiyo nusukaputi ambayo kweli iliipoozesha dunia. Na ndipo tukawekwa humu, tumekata tamaa, kwa sababu kila kiumbe duniani kilitiishwa chini yake. Na kila mmoja iliyezaliwa duniani alitiishwa chini yake.

Kwa hiyo ilipaswa kuja kutoka mahali fulani ambako hakuna dhambi. Isingeweza kutoka duniani. Mmoja wetu asingeweza kumkomboa huyo mwingine. Ilipaswa kutoka kwa mwingine.

Kwa hivyo, mwanadamu alipotambua ya kwamba alikuwa ametenganishwa na Mungu wake, akawa mzururaji. Walilia. Walipaza sauti. Walitaabika. Wakazunguka-zunguka milimani, na katika jangwa, wakiutafuta mji ambao Mwenye Kuujenga na Mwenye Kuubuni ni Mungu. Kwa kuwa, yeye alijua ya kwamba kama angewahi kurudi katika Uwepo wa Mungu, angeweza kuzungumza jambo hilo pamoja Naye. Lakini hakukuwa na njia ya kurudi. Alipotea. Hakujua aelekee upande gani, kwa hiyo alitoka tu, akitangatanga, akijaribu kutafuta mahali fulani ambapo angeweza kupata njia ya kurudi Mahali hapo. Kitu fulani ndani yake kilimwambia ya kwamba alitoka kwenye—Mahali palipo kamili. Hakuna mtu hapa katika wasikizi hawa waliopo hapa asubuhi ya leo, ama katika wasikizi wa kanda za sumaku ambako zitasambazwa duniani kote, hakuna hata mmoja hapa ama po pote pale, ila yule anayeutafuta ule ukamilifu.

20 Unalipia bili zako, unafikiri, "Hilo litamaliza." Unapolipia bili zako, ndipo kuna mtu mgonjwa katika familia yako. Magonjwa yanapokwisha, ndipo una bili nyingi zaidi za kulipa. Punde si punde nywele zako zinapata mvi, ndipo unataka kurudia ujana. Na kuna jambo fulani kila wakati, daima, kwa sababu ya hilo wimbi la dhambi. Lakini moyoni mwako, kwa kuwa unatafuta hilo, inaonyesha ya kwamba kuna ukamilifu mahali fulani. Kuna kitu mahali fulani.

21 Hiyo ndiyo sababu, mara nyingi, siku hizi, mwenye dhambi angali anatanga-tanga. Msichana mrembo atakata vishungi vya nywele zake, apate kupendwa na watu wengi; atajipaka rangi usoni mwake, apate kuonekana mrembo; atavaa nguo kuonyesha maumbile yake. Kwa sababu, ndicho kitu pekee anachoweza kupata, kutafuta mahali fulani kujaribu kupata kitu cha kumrudia, anapoweza kumfanya mwanamume ampigie mluzi, ampungie mkono, afanye ubembe naye. Kijana mwanamume atafanya jambo lile lile kwa mwanamke, akijaribu kujifanya amvutie. Majirani watajenga nyumba, na kuifanyiza namna fulani, kwa sababu itaonekana bora kuliko kwa jirani yake. Ndivyo ilivyo kila wakati, tunatafuta-tafuta kitu fulani, na kitu fulani daima kinaendelea kupanda juu yake kidogo. Huyo kijana mwanamke atapata kumwona kijana mwanamke anayependwa sana na watu kuliko yeye. Jirani atapata nyumba inayoonekana nzuri kuliko yake. Mwanamke huyo atamkuta mwanamke mwingine amevaa namna fulani, ambayo inaonekana vizuri

zaidi kuliko anavyoonekana.

22 Ni kitu fulani ndani yetu, kinachotafuta kitu fulani, na inaonesha ya kwamba tumepotea. Tunataka kupata kile kitu kitakachotutosheleza, kitakachoijaza hiyo sehemu ya njaa mle ndani; lakini inaonekana kana kwamba hatuwezi kukipata. Wanadamu walijaribu jambo hilo katika nyakati zote. Wakakililia. Wakalia machozi. Wakafanya kila kitu walichojua kufanya, bali hata hivyo hawakukipata walipotangatanga ulimwenguni.

23 Hatimaye, siku moja, hiyo ni ile siku pale Kalvari, Mtu mmoja akashuka akaja kutoka Utukufuni. Mmoja, kwa Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyetoka Utukufuni, na Kalvari ikatengenezwa. Hiyo ndiyo siku ambayo gharama ililipwa, na swali la dhambi likatatuliwa milele. Naye akafungua njia ya kitu hiki tunachokionea njaa na kukionea kiu. Ilileta mahali pa utoshelevu. Hakuna mtu aliyepata kutembelea Kalvari na kuona jinsi ilivyokuwa, anayeweza kubaki alivyokuwa. Kila alichoonea shauku au kutamani sana kinapatikana anapofika mahali hapo.

Ilikuwa ni siku muhimu sana, na jambo muhimu sana, liliutikisa ulimwengu. Iliitikisa ulimwengu jinsi ambavyo haujatikiswa hapo awali, Yesu alipokufa pale Kalvari naye akalilipia swali la dhambi, dunia hii yenye dhambi ilitiwa giza kabisa. Jua lilitua mchana nalo likazimia roho kwa wasiwasi. Miamba ikatikisika, milima ikapasuka, miili ya waliokufa ikafufuka ghafla kutoka kaburini.

24 Ilifanya nini? Mungu akalenga shabaha pale Kalvari. Alimjeruhi huyo mnyama, aitwaye Shetani, milele. Sasa yeye amekuwa mkali zaidi tangu wakati huo, kwa sababu ilileta Nuru kwa jamii ya binadamu. Na kila mtu anajua ya kwamba mnyama aliyejeruhiwa ndiye mkali sana, anayetambaa huku amevunjika mgongo. Sasa, Shetani alitupwa nje, pale Kalvari. Dunia ilithibitisha ya kwamba ilikuwa hivyo.

25 Gharama kuu sana iliyopata kulipwa, na Mtu pekee ambaye angeilipia, alikuja na akafanya hivyo pale Kalvari. Hapo ndipo gharama kubwa ilipolipwa. Hilo ni moja ya mambo. Mungu alihitaji hilo. Hakuna mtu aliyestahili. Hakuna mtu aliyeweza. Hakuna mtu angaliweza kufanya hivyo. Ndipo Mungu akaja, Mwenyewe, na akafanyika mwanadamu, na akaishi maisha ya kibinadamu, chini ya tamaa za kibinadamu, na akasulubiwa pale Kalvari. Na pale, wakati Shetani alipodhani kwamba Yeye asingelifanya hivyo, kwamba Yeye asingelistahimili, Yeye aliistahimili Gethsemane na kila jaribu lililowahi kumkabili mwanadamu. Yeye alipitia huko kama watu wote, lakini Yeye akalipa ile gharama

Na hiyo ndiyo iliyoitia giza kabisa dunia nzima Kama ile nusukaputi ya kumtia ganzi mtu anapofanyiwa upasuaji. Daktari anapompa mtu hiyo nusukaputi, kwanza humfanya apoteze fahamu kabla hajafanya upasuaji. Naye Mungu alipolifanyia kanisa u—pasuaji, ulimwengu ulipata nusukaputi, maumbile yakapata mshtuko mkubwa sana. Si ajabu! Mungu, katika mwili wa kibinadamu, alikuwa akifa. Ilikuwa ndiyo saa ambayo ulimwengu ulikuwa umeitazamia, hata hivyo wengi wao hawakuijua.

Kama ilivyo siku hizi, watu wengi wanayatazamia mambo haya, hata hivyo hawayatambui. Hawatambui njia ya kutokea. Wao wangali wanajaribu kutafuta anasa na mambo ya ulimwengu, wakijaribu kutafuta njia ya kutokea.

26 Kumekuwa, na vibao vingi vilivyoelekeza kwenye siku hiyo, vivuli vingi vikuu. Ilikuwa ameoneshwa na kivuli cha mwana-kondoo, na fahali, na hua, na mambo haya yote, lakini hata hivyo yasingeweza kuivunja. Yasingaliweza kuvunja hiyo ngome ya mauti. Kwa kuwa Shetani aliitawala dunia.

Miamba ile ile ambayo wakati mmoja alitembea, juu yake huku na huko duniani, kiberiti kilichowaka moto. Lusifa alikuwa mwana wa asubuhi, naye alitembea duniani wakati ilipokuwa volkeno inayowaka moto. Miamba hiyo hiyo iliyokuwa imepata baridi, wakati Yesu alipokufa Kalvari, ilibubujika toka ardhini.

27 Gharama iliyopwa, na utumwa wa Shetani ukavunjiliwa mbali. Mungu akairudisha mkononi mwa mwanadamu, njia ya kurudia kile alichokuwa akitafuta. Haikumpasa kulia tena. Akapiga, wakati Yeye alipouvunja uti wa mgongo wa Shetani, kule Kalvari, uti wa mgongo wa dhambi, wa magonjwa! Na hiyo ikamrudisha kila mwanadamu, duniani, katika uwepo wa Mungu, huku dhambi zimesamehewa. Haleluya! Dhambi zetu zimesamehewa. Shetani hawezi tena kututia giza akatuondoa kwa Mungu.

Kuna njia kuu iliyotengenezwa. Kuna simu iliyowekwa pale. Kuna simu inayoelekea Utukufuni, inamleta kila mtu karibu na simu hiyo. Kama mtu amejaa dhambi, inamuunganisha na kituo chaa kati. Anaweza kusamehewa dhambi hiyo. Si hivyo tu, bali dhambi hiyo imelipiwa. Loo! Haikubidi kusema, “Mimi sistahili.” Hakika, haungeliweza, kamwe kustahili. Lakini Mtu anayestahili alichukua mahali pako. Wewe uko huru. Haikubidi kutangatanga tena. Si lazima uwe mtu wa kutafuta anasa hapa duniani.

Kwa kuwa damu imebubujika,
Ni ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi walioga chini ya kijito,
Husafiwa kweli.

Haikupasi kupotea. Kuna njia kuu, na Njia, nayo inaitwa Njia ya utakatifu. Mwenye taka haipitii. Kwa kuwa yeye huja kwenye chemchemi, kwanza, kisha anaingia katika njia kuu.

28 Alivunja nguvu za Shetani. Aliifungua milango ya gereza la kuzimu, kwa kila mtu aliyefungiwa, katika dunia hii, katika magereza, akiogopa wakati wa kufa, kile mauti yangefanya kwake. Pale Kalvari, Yeye aliifungua hiyo milango ya gereza, na kumwachilia huru kila mfungwa. Haikubidi tena kunyanyaswa na dhambi. Haikubidi tena kuvitoa viungo vyako kufanya dhambi, kunywa pombe, kuvuta sigara, kucheza kamari, kusema uongo. Unaweza kuwa mwaminifu, mwenye haki, na mnyofu. Wala Shetani hawezi kufanya lo lote kuhusu hilo, kwa kuwa umeshikilia kamba, kamba ya kuokolea, imetiwa nanga katika Mwamba Wenye Imara. Hakuna kitu kinachoweza kukutikisa kutoka Kwake. Hakuna upepo unaoweza kukutikisa kutoka Kwake. Hakuna kitu, hata mauti yenyewe, inayoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu. Hivyo ndivyo Kalvari ilimaanisha.

29 Watu waliokuwa utumwani waliwekwa huru. Watu ambao wakati mmoja walikuwa chini ya hofu ya mauti hawawezi tena kuogopa mauti. Mtu anayeuonea shauku mji, ambao Mwenye Kuujenga na Mwenye Kuubuni, ni Mungu, anaweza kutembea katika njia iliyo kuu, na kuuelekeza uso wake Mbinguni, kwa sababu yuko huru. Haleluya! Yeye amekombolewa. Yeye hahitaji kutangatanga tena, kwa maana kuna njia ya kujua kama uko sahihi au la. Mungu hutupa Uzima. Dhambi zetu zimeondolewa. Siku hiyo pale Kalvari gharama ililipwa. Tunapoona hayo yote, si ajabu mshairi aliandika:

> Huku miamba ikipasuka na anga zenye giza
> Mwokozi wangu aliinamisha kichwa Chake na akafa.
> Pazia lililofunguliwa lilifunua Njia
> Ya furaha za Mbinguni na siku isiyo na mwisho.

30 Haikumbidi Ibrahimu kuendelea kutangatanga zaidi, kote nchini, akiutafuta mji. Mwenye dhambi hapaswi kuwa na wasiwasi tena iwapo ataokolewa au la. Mgonjwa hapaswi kuwa na wasiwasi kama anaweza kuponywa ama hawezi. Pazia iliyofunguliwa, siku hiyo pale Kalvari, ilifunua Njia ya ushindi kamili. Mungu alitupa nguvu za Roho Wake, tupate kuishi tukiwa washindi wa mambo haya yote; tunatakiwa tu kuamini hilo. Hilo lilitukia siku ile pale Kalvari. Hakujapata kuwa na siku kama hiyo. Hakutakuwepo na nyingine kama hiyo. Haihitajiki tena. Gharama ililipwa, nasi tumekwisha kukombolewa. Mungu ashukuriwe! Tumekombolewa. Haikupasi tena kuwa na wasiwasi. Hamna tena kukisia. Zote zimeondolewa. Ile pazia ilifunguliwa pazia, nasi tuko kwenye barabara kuu, tusiwe na wasiwasi tena, bali kuamini na kupiga hatua mbele. Tutatembea hata katika uwepo wa Mungu ulio mkuu.

31 Ibrahimu alijua, na wengine walijua, ya kwamba wakati walipokuwa wakiutafuta ule mji. Walijua walitoka Mahali fulani. Jambo fulani lilikuwa limetukia. Walikuwa wakiishi katika nchi iliyopooza. Matetemeko ya nchi yakaja. Tufani zikaja. Vita na mauaji! Mbwa mwitu na mwana-kondoo wanakulana, ama mbwa mwitu akamla mwana-kondoo, naye simba anamla ng'ombe. Haionekani sawa. Kuna kasoro. Alijua kulikuwa na kasoro fulani. Mwanadamu, ndugu alimuua ndugu, baba akamuua mwana, mwana anamuua baba. Kuna kasoro. Yeye anazeeka. Anakufa. Anatoweka. Maradhi yamo juu yake. Yeye yuko kifungoni. Miti hukua bali si ya kudumu. Inakufa. Milima hubadilika. Bahari hukauka. Maji huisha. Kuna kasoro. Naye akatafuta mahali, mji ambamo hayo hayakutendeka tena. Alijua ya kwamba kama angaliweza kurudi katika uwepo wa yule Mtu aliyeubuni, angezungumza hayo pamoja Naye.

32 Loo, ni majaliwa jinsi gani, mwenye dhambi, asubuhi ya leo kujua ya kwamba umepata njia sasa. Siku hiyo pale Kalvari ilifungua njia. Kwa kuwa hao wazee wetu wote walimtafuta sana Yeye, wakautafuta, Kalvari ilikupa hiyo bure. Unawezaje kuikataa? Unawezaje kuikataa kisha ujiunge na dhehebu? Unawezaje kuikataa, halafu uibadilishe na kitu kingine, anasa za ulimwengu? Kwa nini usikubali jambo hilo? Pazia iliyofunguliwa humleta mtu moja kwa moja ikamrudisha katika uwepo wa Mungu, bila dhambi ya namna yo yote juu yake. Na inaitayarisha njia mbele yake, ya kuelekea kwenye kitu anachokitafuta: Mbinguni, utukufu, amani, uzima wa milele, kila kitu mbele yake.

33 Siku hiyo ilikuwa pigo la ma—mauti kwa nguvu za Shetani. Ilimaliza kila kitu.

Nami naweza kumwona Yeye pale; alikuwa yule Mwana-kondoo wa Edeni, tangu kivuli cha kwanza kilichotokea.

Wakati Habili, kwa imani, alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini. Hapana shaka alikuwa amefunga m—mzabibu shingoni mwa huyo mwana-kondoo, akamvuta hata mwambani. Akatwaa ji—jiwe mkononi mwake, kama kisu, akakivuta kichwa chake nyuma, kisha akamkatakata na kumchonga kwa nguvu hata akafa. Na manyoya yakalowa damu yake. Yeye alilowa kwa damu yake. Ilikuwa ni kivuli.

Bali siku hiyo pale Kalvari, hapakuwepo Mwana-kondoo wa dunia hii, bali ni Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyekuwa anakufa, akagaagaa katika damu Yake Mwenyewe. Alikatakatwa kwa nguvu, akakatwakatwa, akapigwa, akatemewa mate, akatupwa chini, akapigwa makofi, na kufanyiwa kila kitu, na walimwengu, huku damu inatiririka chini ya vishungi Vyake.

34 Wakati mwana-kondoo wa Habili alipokufa, alikufa, akinena katika lugha ambayo Habili hakuweza kufahamu. Alikuwa akilia.

Na Mwana-Kondoo wa Mungu alipokufa siku ile pale Kalvari, Huyo alinena katika lugha ambayo

hakuna mtu alimwelewa Yeye. "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Ilikuwa ni Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyekatwakatwa vipande —vipande, akakatwakatwa.

Yeye alikuwa Mwana-Kondoo yule yule ambaye Habili alikuwa naye akilini, wakati alipoona Uzao ulioahidiwa wa mwanamke. Yeye alikuwa Mwana-Kondoo ambaye Danieli alimwona, aliyechongwa kutoka mlimani, bila mikono. Yeye alikuwa Gurudumu katikati ya gurudumu, kwa ajili ya nabii. Yote waliyokuwa wameyaona yalitimizwa siku hiyo, siku hiyo pale Kalvari. Hilo liliingiza kile kitu kikuu. Hiyo ilimvunja Shetani mgongo.

35 Kwanza, inatupasa kutafuta kujua maana ya siku hiyo. Pili, inatupasa kuona yale hiyo siku iliyotufanyia, sasa vile ilivyotufanyia. Sasa, ya tatu, hebu na tuone yanayotupasa kuifanyia siku hiyo. Tunapaswa kufanya nini?

Kwanza, inatupasa kuichunguza, kwa kuwa ni siku kuu, siku iliyo kuu kuliko siku zote. Gharama ya dhambi ilimalizika. Nguvu za Shetani zilivunjwa.

Na sasa tunataka kuona kile tunachopaswa kufanya katika kurudi. Sasa mahali pake, Yesu alipokufa msalabani, pale Kalvari siku hiyo, Yeye hakulipa tu gharama ya dhambi zetu, bali alilipa gharama hiyo na pia akatufanyia njia tupate kumfuata Yeye; kwa maana sisi, kama Adamu aliyeanguka ambaye amekombolewa, Kama Roho alivyomwongoza Adamu (Adamu wa kwanza) kwa Roho, ambaye alikuwa na mamlaka juu ya maumbile yote, ndipo sisi (Adamu wa pili), ama watu wa duniani tumekombolewa na Kristo, tangu siku hiyo pale Kalvari, tunaweza kumfuata Yeye. Sasa, wakati alipokufa pale Kalvari, alifanya njia. Alitoa Roho, Roho Mtakatifu, ambaye alimtuma arudi duniani, kwa ajili yako na mimi tupate kuishi kwake. Hiyo ndiyo maana ya Kalvari kwetu, kumfuata Yeye.

36 Kwanza, ichunguze, uone iliyotutendea Na sasa tunapaswa kufanya nini kuhusu jambo hilo? Ni lazima mimi na wewe tufanye nini?

Sasa, tunasema, "Vema, ni—ninathamini jambo hilo. Hilo ni zuri sana." Lakini hatuna budi kuyakubali. Na kuyakubali ni kuikubali nafsi Yake, Kristo, mioyoni mwetu.

Ndipo, tunakuwa huru na dhambi, kwa hiyo, hakuna kabisa pingu za dhambi zinazoning'inia, kwetu. Mungu, kama tu kwamba hatukuwahi kutenda dhambi, Ile sadaka iliyo kamilifu ilitufanya wakamilifu. Kwa kuwa, Yesu alisema, "Kwa hiyo iweni wakamilifu, kama Baba yenu aliye Mbinguni alivyo mkamilifu." Halafu, hakuna zaidi ya kufanywa, bali tunakamilishwa Mbele za Mungu.

37 Sasa, hapo ndipo tunapopoteza nafasi yetu. Kama hatuangalii, tunajaribu kuangalia nyuma kwenye kile tulichokuwa. Na mradi tu tunatazama nyuma kwenye kile tulichokuwa, Dhabihu haina maana kwetu. Loo, hivi hamwezi kuliona, kanisa? [Kusanyiko linasema, "Amina. — Mh.] Nisingeweza … Nisingejaribu kazi hiyo. Siwezi, na wewe pia huwezi. Hakuna haja ya kujaribu. Umepotea, kwanza, mradi tu unaangalia yale uliyofanya. Lakini usiangalie yale umefanya.

Angalia kile siku ile pale Kalvari ilichokutendea. Ililipa gharama yako. Ilimaliza lile swali. Dhambi zako ziwe nyekundu sana, zinakuwa nyeupe kama theluji. Nyekundu kama bendera, nyeupe kama sufu. Basi huna dhambi. Wewe huna dhambi kabisa. Haidhuru umefanya nini, ama ufanye nini, ungali huna dhambi. Mradi tu umemkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako, dhambi zako zimesamehewa. Cho chote *kilichosamehewa* "kimeondolewa na kusahauliwa".

Ndipo inafanya nini? Inakupa wewe baada ya hali hiyo Roho Wake kumfuata, na kufanya kama ilivyofanya, kwa wengine wanaofuata. Yeye alikuwa ni Mtu mmoja tu, Mtu mkamilifu. Alitoa uhai Wake, naye alitoa mfano kwako. Sasa tunapaswa kufanya nini?

38 Sasa, jambo la kwanza ninalotaka kusema, ni, Yesu kamwe hakuishi kwa ajili Yake Mwenyewe. Maisha yake yalitumika kwa ajili ya wengine. Huo ni uzima wa milele hasa. Unaposema unaenda kanisani, na unafanya mambo mazuri, hilo ni sawa. Bali unapojiishia maisha yako binafsi, hauna uzima wa milele. Uzima wa Milele, ni kuishi kwa ajili ya wengine. Ilithibitika alipokuja Mwana-Kondoo wa Mungu. Aliishi na alikuwa na uzima wa milele kwa sababu, Yeye hakujiishia Yeye Mwenyewe. Yeye aliishi kwa ajili ya wengine. Nawe unapokea Uzima wa Milele, kwa kuipokea siku hiyo, wala huishi kwa ajili yako mwenyewe tena. Unaishi kwa ajili ya wengine.

39 Mtu fulani alisema, "Unawezaje kusimama, kumwacha mtu ye yote akuite majina mabaya namna hii?" Huishi kwa ajili yako mwenyewe. Unaishi kwa ajili ya wengine, upate kumkomboa mtu huyo. Mnafanyika wana. Na shida yake ni kwamba, kanisa limesahau ya kwamba wao walikuwa wana. Ninyi ni wana. Mnapachukua mahali pa Kristo. Ninyi ni wana; kwa hivyo msijiishie wenyewe. Waishieni wengine.

"Vema, Ndugu Branham, naweza kumwishia ndugu huyu kwa sababu yeye ni mtu mzuri sana." Si hivyo.

Ishi kwa ajili ya mtu huyo anayekuchukia. Mwishie mtu huyo ambaye angekuua kama angeweza.

Hivyo ndivyo walivyomtendea. Walimwua, Naye akafa, apate kuwaokoa. Huo ni Uzima wa Milele. Unapoupata, huo ndani yako, unaelekea Mbinguni wakati huo. Lakini toa dhabihu vitu vyako, vitoe kama mwana-kondoo anavyotoa manyoya yake. Unaangalia, kuelekea Kalvari.

40 Natumaini hili litakusaidia kufikia mahali fulani. Hivyo ndivyo Maskani haya, hivyo ndivyo watu wote, wanapaswa kufanya, ni kujua ulivyo, na kusudi lake ni nini. Kanisa, si kwenda kanisani kupiga tu muziki, kuimba nyimbo. Kanisa ni mahali pa masahihisho. "Hukumu huanza katika nyumba ya Mungu."

"Lazima tujihesabu wafu, na walio hai kwa Kristo." Ndipo, Yeye alitengeneza njia ambayo tungeweza kujitolea kwa ajili ya utumishi Wake, kumfuata Yeye. Kama tukimfuata Yeye, tunaishi maisha aliyoishi Yeye. Hilo ni zuri sana.

41 Yesu alisema, na kunena habari zake. Hebu niwape tu nukuu chache juu yake. Sikilizeni kwa makini. Usilikose. Yesu alisema, kwenye Siku hiyo Yeye angewatenga watu, kama kondoo na mbuzi. Naye angewaambia mbuzi, "Simameni upande wa kushoto." Na kwa kondoo, "Simameni upande wa kuume."

Naye akawaambia wale mbuzi, "Ondokeni Kwangu. Kwa sababu, nilikuwa na njaa, wala hamkunilisha Mimi. Nilikuwa kifungoni, msije kunitazama. Nilikuwa uchi, msinivike nguo. Nilikuwa na kiu, msininyweshe. Nilikuwa mgonjwa, msije kunitazama. Kwa hiyo, ondokeni Kwangu."

Na upande wa kondoo, alisema, "Nilikuwa na njaa mkanilisha. Nilikuwa uchi mkanivika. Nilikuwa mgonjwa, nanyi mkanihudumia."

Na angalia. Msikose kulipata hili, kanisa!. Liwekeni hili mioyoni mwenu milele. Yalitendwa bila kujua kabisa. Watu hawafanyi hivyo kama jukumu lao. Mtu anayekupa kitu fulani kwa sababu anapaswa kufanya hivyo, mtu anayekulisha kwa sababu inampasa kufanya hivyo, ana wazo la kichoyo. Inapaswa kuwa maisha yako halisi, matendo yako halisi.

42 Iliwashangaza sana hawa kondoo hata wakasema, "Bwana, ni lini ulipokuwa na njaa tusikulishe? Nasi tusingekulisha … Ni lini ulipokuwa na njaa, tukakulisha? Ni lini ulipokuwa uchi, tukakupa nguo? Ulikuwa na kiu lini, tukakunywesha? Ni lini ulikuwa mgonjwa, tukakuhudumia?"

Yalifanywa bila kufikiria kabisa kwa upendo, ni maisha yao waliyoishi. Mungu jalia watu waone kile Kalvari ilichotufanyia.

"Ni lini ulikuwa, Bwana? Hatukujua kamwe jambo hilo."

Angalia kile Yesu alichogeuka na kusema, "Kadiri mlivyowatendea hawa, mlinitendea Mimi."

Maisha yasiyo na ubinafsi; si wazo la pili. Si kuliwazia; bali umekufa kabisa kwa mambo ya ulimwengu huu, uko hai kabisa katika Kristo, na unatembea imara kwenye ile njia kuu, hata mambo haya yanatukia yenyewe tu. Unatenda tu. Si kusema, "Vema, sasa, Bwana angetaka, Bwana, anitaka nifanye hivyo." Si hivyo. Wewe ni sehemu Yake tu. Roho Wake yuko ndani yako, nawe unatenda jinsi Yeye alivyotenda. Ah! Unalipata.

43 "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti."

"Si wote wasemao, 'Bwana, Bwana,' watakaoingia, bali ni wao wafanyao mapenzi ya Baba Yangu," kutoka tu mioyoni mwao, kwa unyofu tu.

Sasa, siku hiyo pale Kalvari ililipia gharama hiyo, ili tuweze kuwa hivyo.

Si kusema, "Unajua, mjane Jones wakati mmoja alikuwa ... Hakuwa na mkaa, nami nikaondoka nikaenda nikamnunulia makaa kidogo. "Nakwambia, nalimwona ndugu aliyehitaji suti, nami nikaondoka nikaenda nikamnunulia suti. Mungu abarikiwe! Mimi ni Mkristo." Loo, jamani! Ewe mtu mchoyo, maskini, mwenye mashaka. Ninyi ni wanafiki.

"Usiache mkono wa kulia ujue yale wa kushoto unalofanya, wala wa kushoto usijue wa kulia unalofanya." Umekufa kabisa katika Kristo, hata utalitenda, kwa vyovyote. Ni asili yako. Ndivyo ulivyoumbwa. Utafanya hivyo, kwa vyovyote. Ni uhai tu unaoishi ndani yako. Umejitoa kabisa kwa Roho huyo, naye Mwenyewe anaishi maisha Yake ndani yako. Loo, unamsikia huyu Roho aliyebarikiwa, huo uhai! "Si mimi niliye hai," kasema Paulo, "bali Kristo yu hai ndani yangu," inatukia hivyo tu.

44 "Vema, nakwambia, Ndugu Branham, sisi ni Wakristo hapa. Tunawasaidia watu *hawa*. Tunawasaidia watu *hao*." Loo, jamani! Aibu kwako. Huo si Ukristo.

Ukristo ni tukio linalotendeka tu. Linapaswa kufanywa. Nawe unasahau tu kuhusu, yote kuhusu, "Mimi siko." Nenda, ukafanye hivyo.

Kristo aliyakabidhi kikamilifu maisha Yake kwa Mungu. Yeye alijitoa, kama mtumishi wa umma, kwa watu. Yeye alitoa uhai Wake, bure. Haikumlazimu kufanya hivyo. Yeye hakufanya hivyo kwa kinyongo.

Hakusema, "Sasa, ndugu, nyote yawapasa kunifikiria sana Mimi, kwa sababu nilikuja kuwafia ninyi." Kamwe hakusema neno juu yake. Yeye alikufa, hata hivyo, kwa sababu ilikuwa ni Mungu ndani Yake.

Ni Mungu ndani yako, ni Mungu ndani yangu, anayetufanya tuwaangalie wengine. Kondoo, upande mmoja.

45 Mmoja wao atasema, "Naam, Bwana, nalifanya *hili.* Na Bwana, nalifanya *hilo*."

Yeye alisema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Sikuwajua ninyi kamwe."

Laiti kanisa lingefikia kweli hizo za kimsingi, hilo si jambo unalojaribu kufany, wewe unajitahidi kufanya hivyo. Ni kitu ulichozaliwa nacho.

46 Samahani, marafiki zangu Wapentekoste. Mimi ni mpentekoste. Lakini marafiki zangu Wapentekoste wamefikia mahali, ambapo inabidi kuwe na muziki moto moto, bendi fulani ikiimba, ama kupiga makofi, ama matari kusababisha vifijo. Huo ni msisimuko tu. Watu hucheza bendi kabla hawajaenda vitani. Kuwaingiza watu katika msisimuko wa vita. Ninaamini katika muziki. Ninaamini katika kupiga makofi. Lakini ninaamini katika mambo haya. Hiyo ni kweli kabisa. Tunapaswa kuwa na jambo hilo.

Lakini mmeacha mambo makuu bila kuyafanya, ni hayo maisha ya kujitoa mwenyewe ambayo Mungu anaishi ndani yako, ukitenda bila kufikiria tu yaliyo haki, kwa sababu ni haki Kuendelea tu, hata usifikiri cho chote juu yake. Unaishi hivyo tu. Halafu angalia, unaona yanayoendelea. Unaninii tu … hauninii … Uko kwenye njia kuu. Hivyo ndivyo Kalvari ilimaanisha kwako, kwenye njia kuu, iliyofunguliwa kwa ajili yako siku hiyo.

47 Sasa, sasa kumbuka, huwezi kuwa nusu mbuzi na nusu kondoo. Hawawezi kuchanganyika.

Sasa, kuna watu wengi wanaosema, "Naam, unajua nini? Tuna madhehebu katika kundi letu. Sisi, tunawasaidia maskini. Tunafanya jambo *hili*." Hiyo ni sawa, lakini unajigamba. Usifanye hivyo.

"Toa sadaka zako katika siri," Yesu alisema. Kwako ni jambo tu, unalotenda bila kufikiria, si tofauti na kwenda, ukachukua maji ukanywa. Unakuwa na kiu. Kama mtu aliye karibu nawe ana kiu, mfikirie, pia. Mahitaji ya mtu aliye karibu na wewe, mfikirie jinsi tu ungelifikiria mahitaji yako. Na usijali. Endelea kuishi tu.

Sasa, huwezi kuwa nusu kondoo na nusu mbuzi.

48 Kwa hiyo kama ukisema, "Vema, kanisa letu lina madhehebu. Tunawapa maskini, na tunafanya *hivi*, na kufanya *vile*, na kufanya *vingine*."

Kama ulikuwa na hilo bila lile jingine, Maisha ya Kristo ndani yako, unayofanya ni ubatili mtupu. Yesu … Paulo alisema katika I Wakorintho 13, "Nijapotoa mali zangu zote kuwalisha maskini, na kuutoa mwili wangu niungue moto kama dhabihu, si kitu mimi."

49 Sasa, hili ni gumu, bali ni Kweli. Huna budi kufikia jambo hilo, kutambua yale Kalvari iliyokufanyia. Tunaliangalia, na kusema, "Loo, naam, hilo ni sawa." Hilo silo. Kama huyo Mwana wa Mungu ilibidi aende Kalvari, kwa ajili ya kusulubiwa, kila mwana ajaye hana budi kwenda Kalvari. Yeye hana budi kuwa na Kalvari pia. Huna budi kuwa na siku hiyo ya Kalvari. Sina budi kuwa na siku hiyo ya Kalvari. Hilo latatua swali la dhambi. Si kupeana mikono na mhubiri, si kupewa mkono uingizwe kanisani, si kuingia kwa barua, si kuingia kwa kukiri. Bali kuingia kwa kuzaliwa. Kamwe hakutoa barua. Yeye hakutoa kukiri. Yeye alitoa kuzaliwa. Hivyo ndivyo tunavyoingia. Ndipo, kutokea hapo, tunaishi maisha ya Kikristo moja kwa moja.

50 Sasa, tamshi lingine. Nusu mbuzi, nusu kondoo, hawana kitu kama hicho. Wewe ama mbuzi au kondoo. Wewe si nusu mbuzi na nusu kondoo. Wewe ama mbuzi au kondoo.

Sasa, kama unafanya tu mambo mazuri, na unafikiri unaweza kuingia, kwa jambo hilo, basi hakungepaswa kuwa na siku ya Kalvari. Torati ilikuwa na hayo. Lakini sababu ya siku ya Kalvari, kuhitajika ni kuingiza hilo ndani, kusudi tusiwe tu washiriki wa kanisa, bali tuwe wana wa kiume na wa kike wa Mungu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa siku ya Kalvari. Hivyo ndivyo ilivyomaanisha kwako, kusudi ufanye, umfuate, na utende kama Yesu.

Sasa, mto hautiririki kuelekea juu na kuelekea chini, wakati ule ule. Mto hutiririka kuelekea upande mmoja tu. Naye Roho wa Mungu huelekea upande mmoja. Hajichanganyi na mambo. Huelekea upande ule ule.

51 Mtazameni Yesu, tunapofunga. Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, na kubwa kuliko hizo mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba."

Sisemi jambo hili sana kwa kanisa hapa. Mnaelewa. Lakini Jumbe hizi zinarekodiwa. Makumi ya maelfu wanawasikia, kote ulimwenguni.

Nitajibu swali hilo kwa mkosoaji, sasa hivi. Mara nyingi nimesemwa … nimeambiwa. Wanasema, "Mbona, unaamini Biblia? Yesu alisema, 'Kazi hizi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, na kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu.'"

52 Unaweza kuwa mbaya jinsi gani, bwana? Unaweza kutangatanga mbali na upambanuzi jinsi gani, kwa hekima ya theologia yako, kwa mawazo ya akili yako juu ya jambo lo lote? Rafiki yangu mwema uliyepotea, je hauwezi kufahamu ya kwamba Biblia hii inafasiriwa kiroho?

Yesu alimshukuru Baba kwamba Yeye alikuwa ameyaficha hayo kwa wenye elimu, watu werevu, wenye hekima, na akili, naye atawafunulia watoto wachanga ambao wangekuja Kalvari.

53 Sasa angalia. Yesu alisema. Angalia jinsi alivyolisema. "Kazi nizifanyazo," Yeye anazifanya sasa hivi. "Kazi ninazofanya sasa, kuwaponya wagonjwa, kuwafufua wafu, kuyafungua macho ya vipofu, kazi hizi mtazifanya pia. Mtafanya haya kama mkiniamini Mimi. Mtazifanya hizi kazi. Na halafu kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu."

"Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Sitawaacha ninyi yatima. Nitamwomba Baba, Naye atawapelekea Msaidizi mwingine, ambaye ni Roho Mtakatifu, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, bali ninyi mnaweza kumpokea Huyo."

54 Sasa angalia. Sasa tazama zile kazi kubwa zaidi zilikuwa kupata nguvu kanisani, si kuwaponya tu wagonjwa kwa maombi, kuwatoa pepo kwa maombi, bali kuwapa waamini uzima wa milele. Roho Mtakatifu alikuwa yuaja na aliwekwa mikononi mwa kanisa apate kuwapa Uzima. Loo! Hiyo ndiyo maana ya Kalvari. Alichukua wanaume na wanawake waliodhiliwa na walioshushwa vyeo naye akawainua mpaka mahali, ambapo wamekuwa wana na binti za Mungu, kuwaponya wagonjwa na kuwapa uzima wa milele; kwa kuwapa Roho Mtakatifu waaminio watiifu, watu ambao siku moja walikuwa wasioamini, kuwafanya waamini, na kuwapa uzima wa milele. Ni kuu zaidi kiasi gani, kumwambia ...

55 Mwanamke huyu mgonjwa anayelala hapa, naweza kuomba ombi la imani naye ataponywa. Hilo ni jambo kuu. Hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya wakati huo.

"Bali" akasema, "Kubwa kuliko hizi mtazifanya. Nitawapa nguvu, si kumwinua juu tu kwa muda kidogo, bali kumpa Uzima wa Milele, ambao utakuwa wa milele na milele." Watu maskini, vipofu, wanyonge, mnakosaje hilo? Je, hamuoni hilo jambo "kuu" ni nini? Hilo ndilo jambo kuu sana ambalo lingaliweza kutendeka, lilikuwa kuwapa watu Uzima wa Milele. Uzima wa Milele ni nini? Maisha aliyoishi Yeye, Uhai uliokuwa ndani Yake, kuwapa huo wengine. Mtu anaweza kufanya hivyo? Mwana wa Mungu anaweza.

56 Yesu alisema, "Wo wote mtakaowaondolea dhambi wameondolewa, wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa."

Sasa, hapa ndipo Kanisa Katoliki na mengine mengi yalitenda kosa lao kubwa. Wao wanaondoka na kusema, "Nakusamehe dhambi zako." Haikuwa hivyo.

Je, hao walisamehewa dhambi zao vipi, katika Biblia? Petro alijibu swali hilo, kwenye Siku ya Pentekoste. Walisema, "Tufanye nini tupate kuokolewa? Tunawezaje kupata Hili ambalo ninyi nyote mnalo?" Yeye aliweka maagizo. Aliwaambia la kufanya.

Yeye alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, kwa Mungu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Kwa nini? Kwa Ondoleo la dhambi zenu. Ndizo hizo zile kazi *kubwa*.

57 Ni wangapi, wenu wahubiri asubuhi ya leo, ni wangapi wenu mnaosikiliza asubuhi ya leo, ni wangapi wenu mnaosikiliza neno langu kwenye kanda ya sumaku, je, mko tayari kwenda Kalvari asubuhi ya leo? Na angalia yale Mungu aliyofanya pale kwa ajili yako. Na kuacha kanuni zenu za kimadhehebu, na kuihubiri Injili. Haleluya! Liko kwenye paja lako sasa. Utafanya nini nayo?

Habari ya toba na ondoleo la dhambi lazima kuhubiriwa katika jina Lake, ulimwenguni kote, kuanzia Yerusalemu." Haleluya! Utukufu! Haya basi.

Kalvari ina maana gani kwako? Siku hiyo ingekufanya nini? Je, ilikujaza theolojia chungu nzima? Je, ilikufanya mwenye kiburi? Ama ilikufanya Mkristo, aliyejitoa kabisa? Haleluya!

Dhambi, ikaondolewa! "Kazi kubwa kuliko hizi mtazifanya." Mnaona mahali akina *ninyi* walipo, sivyo? "Kazi kubwa kuliko hizi," kuondoa dhambi, katika jina la Yesu Kristo.

58 Lakini kupitia kanuni za imani, na madhehebu, na kadhalika ulifungwa sana hata kufikia mahali, ambapo ungali unautumikia ulimwengu. Niambieni mwanaume ye yote, niambieni mwanamke ye yote, anayeweza kuja Kalvari na kujaribu kuwa mtu mashuhuri kwa sababu mtu fulani alisema jambo fulani. Niambie ni wapi unakoweza kutazama uso wa Kalvari, katika nuru yake iliyo sahihi, siku hiyo katika Kalvari. Unawezaje kuwa na siku yako pale Kalvari, kisha utoke mtu mwenye majivuno? Wawezaje kutoka

huko ukiwa kibaraka wa madhehebu fulani, kuhubiri mafundisho yaliyobuniwa na mwanadamu? Mbona isikufanye mnyenyekevu kwa Neno la Mungu? Ukienda pale, utatoka ukiwa mnyenyekevu. Wawezaje kutamani kuwa mtu fulani mkuu katika dhehebu lako ukiwa na majivuno, huku Kristo, Mwana wa Mungu alijinyenyekeza hata akakatakatwa mwili, na kutemewa mate usoni, hata aibu na fedheha. Nao walimvua nguo Zake, na kumsulubisha, mbele ya ulimwengu. "Kudharau aibu." Wawezaje kwenda katika Kalvari na utoke ukiwa kitu tofauti na vile Yeye alivyokuwa, fedheha, aibu?

"Loo," unasema, "watanifukuza." Hebu na wakufukuze.

Pata siku yako kule Kalvari, Mungu atajua la kukutendea. Hebu ninukuu jambo hilo tena. Pata siku yako kule Kalvari, Mungu atajua la kukutendea.

Hebu na tuombe.

59 Bwana, Ee Mungu, tupeleke sote Kalvari sasa hivi. Hebu na tutoke katika ubinafsi, Bwana, kumwogopa mwanadamu, kuogopa yale mtu fulani atakayosema. Mbona, ulimwengu wote ulimcheka, ukamdhihaki. Lakini Yeye alikuwa mtiifu, hata mauti. Alikuwa mtii hata, fedheha. Yeye alikuwa mtiifu, hata chini ya serikali ya shirikisho.

Nasi tunatambua ya kwamba Shetani alipoipiga dunia hii, alifanyika mtawala na mwenye mamlaka katika dunia hii. Alishuhudia jambo hilo mbele ya Bwana wetu, akasema, "Milki hizi ni zangu. Nitazifanyia kama nipendavyo." Nasi tunatambua ya kwamba, tangu siku hiyo hadi leo hii, ulimwengu huu, chini ya laana, umetawaliwa na yule aliyeulaani.

Lakini, Mungu, Ee Mungu, tunautumikia Ufalme ambao haujalaaniwa.

Baba Mungu, ni ajabu vipi kwamba umefanya mambo makuu katika ulimwengu wa—wa sinema siku hizi. Ukiruhusu sinema hizi za mambo makuu, kama *Amri Kumi*, na kadhalika, zitokee, ukawaruhusu wanaume na wanawake kuziona, ambao hata hawangalithubutu kuingia katika mlango wa kanisa, bali ukawaruhusu waone vile zilivyo. Njia ya Mungu ni njia iliyokataliwa, na ulimwengu. Kwa sababu sisi ni kama … Tunaingia Urusi chini ya ukomunisti.

Tuko katika ulimwengu huu, bali sisi si wa ulimwengu huu. Tumekwisha kwenda Kalvari. Tumejisulubisha, pamoja na ufalme wa Mungu, kuwa mmoja wa hao walio Wake. Haidhuru ulimwengu utasemaje, tunaungana na wale wachache wa Mungu waliodharauliwa. Tunapiga hatua kuelekea ule ufufuo, nasi tunaamini umekaribia sana, Bwana, wakati tutafufuliwa katika ufalme utakaoutwaa ulimwengu huu. kama Danieli alivyouona awali, na Yeye akauvunjilia mbali ulimwengu, vipande-vipande, kama makapi ya sakafu za kupepetea wakati wa hari na upepo ukavipeperusha. Bali, ule mlima, lile jiwe likakua likawa mlima mkubwa ulioijaza dunia. Hilo Jiwe litakuja. Ee Mungu, tunataka kuwa sehemu yake. Hebu na tujikane, tuchukue msalaba wetu kila siku, tumwishie Kristo, tuishi kwa ajili ya wengine. Tujalie, Bwana.

60 Kama kuna baadhi ya watu hapa asubuhi ya leo wasiomjua Yeye kama Mwokozi, nao wangetaka kukumbukwa katika maombi ya kumalizia, na wangetaka hii iwe siku yao pale Kalvari, waweza kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham. Ninataka kumjua kama Mwokozi wangu." Mungu akubariki, ewe kijana. Mtu mwingine? Mungu akubariki, ndugu yangu huko nyuma.

Kungekuwako na mtu mwingine? Sema, "Ninataka kumjua Yeye. Nataka hii iwe siku ya pale Kalvari, kwa ajili yangu. Mimi ni mgonjwa na nimechoka. Kuna faida gani kwangu kufanya mchezo hapa na kitu halisi nilichozaliwa kufanya? Nilipozaliwa, nilizaliwa kuwa mwana wa Mungu, na mimi niko hapa nikiyashikilia mambo ya ulimwengu. Mungu, hebu nisulubiwe leo. Hebu nijisulubishe, leo, pamoja na mawazo yangu, nipate kuishi pamoja na Kristo, na nipate kuwaishia wengine. Haidhuru watanifanyaje, hata wakinidhihaki, wakinitesa, na kusema maovu yote dhidi yangu, na kadhalika, hebu nitembee kwa unyenyekevu, mnyenyekevu kama mwana-kondoo, kama Yeye alivyofanya. Na siku moja, Yeye ameahidi kunifufua tena, kwenye Siku ya mwisho. Ninaitazamia Siku hiyo." Je, kuna mikono mingine itakayoinuliwa? Mungu akubariki huko nyuma, na wewe. Vema. Wengine zaidi tu … Mungu akubariki. Mungu akubariki. Wengine kabla hatujaomba.

61 Baba yetu wa Mbinguni, ilisemwa, wakati Petro alipohubiri kwenye Siku ya Pentekoste, "Wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa." Kwa kweli waliamini kwa mioyo yao yote. Watu hawa ambao wameinua tu mkono wao, ninaamini ya kwamba wameamini kwa moyo wao wote. Na kama wamefanya hivyo, kuna kidimbwi cha maji kinachongoja hapa. Wanataka dhambi hizo zisamehewe. Kuna mtu hapa anayeweza kuwabatiza katika Jina hilo, na Jina pekee lililo chini ya Mbingu walilopewa wanadamu, ambalo hatuna budi kuokolewa.

Kwa kuwa, kama nilivyonukuu Maandiko dakika chache zilizopita, ya kwamba, "Toba na ondoleo la dhambi havina budi kuhubiriwa katika Jina Lake, kwa ulimwengu wote, kuanzia Yerusalemu." Na kule Yerusalemu, wakati toba na ondoleo la dhambi lilipohubiriwa, mtume aliwaambia Maandiko, na kusema, "Wao hawana budi kutubu, kwanza, kisha wabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Hiyo ndiyo iliyokuwa kazi

ya wahubiri. Ili wao watubu, na yeye awabatize kwa ondoleo la dhambi zao. "Wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa, wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa."

62 Baba, walimwengu walipatwaje na hamaki waliyo nayo? Mbona wasiamini injili iliyo rahisi? Nao hata huingiza kwa ajili ya hiyo kutia majina ya uongo badala yake, mabatizo ya uongo, ubatizo wa uongo wa Roho Mtakatifu, kupeana mikono na wahudumu, wakitumia vyeo vya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ambao haupo katika Maandiko; mpango uliewekwa na watu wa Kirumi, si mafundisho ya Kikristo hakuna mahali po pote katika Biblia. Kuondolewa kwa dhambi hakuwezi kuondolewa kupitia cheo, bali kwa Jina la Yesu Kristo.

Sasa, Baba, tunajua jambo hilo halipendwi sana. Njia zako daima zimekuwa hivyo. Lakini hebu wanaume na wanawake, asubuhi ya leo, wafikie siku hiyo, siku hiyo pale Kalvari. Ambapo, Yesu, akiidharau siku hiyo, aibu hiyo, ya kuvuliwa nguo, kukatwa vipande-vipande, kutemewa mate, na kudhihakiwa, na ulimwengu mzima, na kanisa, na watu waliostahili kumpenda. Na, hata hivyo, katika yote hayo, Yeye hakufungua kinywa Chake, na akaenda akawafia hao watu waliokuwa wakimdhihaki.

63 Mungu, tupeleke Kalvari asubuhi ya leo. Na kama wakisema sisi tuna kichaa, wanasema tunakosea Maandiko, lo lote wanalotaka kusema, Mungu, hawawezi kusimama Mbele za Mungu na kusema ni makosa.

Hawawezi kufunika dhambi zao kwa Biblia. Biblia inafunua dhambi zao: kutokuamini kwao; kuwa maarufu; kufanya kama umati uliosalia. Hebu na waje Kalvari asubuhi ya leo.

"Na kuanzia Yerusalemu; ya kwamba toba na ondoleo la dhambi hazina budi kuhubiriwa katika Jina Lake kwa mataifa yote, kuanzia Yerusalemu."

Hebu na wazichukue hatua zile zile za kusulubishwa wakatwe-katwe; na kutemewa mate, wadhihakiwe, na kuitwa cho chote wanachoweza kuitwa kama wanaobadili dini zao; wanaoyavunja makanisa, yote wanayotaka kuwaita.

Tujalie nasi, Bwana, asubuhi ya leo tuungane na wachache wa Bwana wanaodharauliwa. Tujalie tutembee kama walivyofanya mitume, tusigeukie upande wa kulia ama kushoto, na kwa unyofu wa mioyo yetu tumtumikie Mungu. Jalia hilo, Baba.

Sasa, waponye wagonjwa na wanaoteseka wanaoingia kwenye mstari wa maombi. Jalia hawa wanaoinua mikono yao, mioyoni mwao, watubu, sasa hivi. Hebu wale waliosimama nyuma muda mrefu sana, haraka wahamie majini na kusamehewa dhambi zao juu ya Jina la Dhabihu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Chini pale msalabani Mwokozi wangu alipofia,
Chini pale nilililia utakaso toka dhambi;
Pale moyo wangu ulipopakwa Damu;
Utukufu kwa ninii Yake …
Utukufu kwa Jina Lake!
Loo, utukufu kwa Jina Lake!
Loo, Pale moyo wangu ulipopakwa Damu;
Utukufu kwa Jina Lake!
Nimeokolewa kutoka dhambini kwa njia ya ajabu mno, (Jinsi gani?)
Yesu hukaa ndani yangu kwa upendo,
Pale msalabani Yeye alipo … (Kuwa mmoja wa Wake.) niingiza;
Loo, litukuzwe Jina Lake!
Litukuzwe Jina Lake!
Litukuzwe Jina Lake! (Jina la thamani.)
Loo, pale … moyo ulipopakwa Damu;
Jina Lake litukuzwe …

Je! Hilo halifanyi jambo fulani kwako? Linakusafisha tu. Huweka tumaini ndani yako: Uzima, Uzima wa Milele.

Ni nini "kusulubiwa pamoja na Kristo"? Ni kuishi kwa ajili ya wengine. Ni watu wa aina gani? Wale wanaokuchukia, wale wasiokupenda, wale ambao wangekufanyia mzaha: waishie; kuwa pamoja nao; wapendeni; "waombeeni wale wanaowatumia vibaya, wanaosema kila namna ya uovu kwa uongo, kwa ajili ya Jina Langu. Waliwatesa manabii waliokuwako kabla yenu."

Nilifikiri ujumbe huo labda ungesaidia kanisa asubuhi ya leo, kwamba mngeona ya kwamba tunahitaji Kalvari, tunahitaji kusulubishwa.

Sasa yote yamefanywaje? Yote yamelipiwa. Dada katika kiti cha magurudumu, kwa watu hapa walio wagonjwa na wanaoteseka: Yote yamelipiwa; jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuamini ya kwamba ni yako; likubali kwa njia ile ile, nawe utaponywa.

Kumbuka: Sasa ni kitu gani? Ungeweza kwenda ulimwenguni, kuhubiri Injili, kuwaponya wagonjwa; na kutoa Uzima wa Milele.

Ingekuwa ni kubwa zaidi iliyoje: ya, huyu hapa mtu amelala hapa mwenye—mwenye uvimbe, kansa, cho chote kile. (Tumemwona mara nyingi sana akitoa baraka Zake na kumponya mwanamume, kumponya mwanamke; makumi ya maelfu mara maelfu ya visa visivyoweza kukosea kote ulimwenguni, mnaona, aliwatoa kwenye vitanda, machela; kivuli tu cha watu kilicholiwa na kansa. ; leo, watu wazuri, wenye afya.) Kazi hizi nizifanyazo mimi ninyi nanyi mtazifanya; lakini kubwa kuliko hili mtafanya; "Zaidi ya hizi," ni kweli.

Nini? Niliwapa nyongeza ya maisha, kwa Jina la Yesu, kuyaendeleza maisha yao kwa siku chache.

Lakini, "Zaidi ya haya mtafanya: mtawapa Uzima wa Milele kwa Jina Langu." Whiu!

Kwa nini uonee haya Jina hilo la thamani? Kwa nini watu walionee aibu na kuliondokea? Ni Ibilisi. Hakika.

"Toba na ondoleo la dhambi havina budi kuhubiriwa katika Jina Lake ulimwenguni kote, kuanzia Yerusalemu." Hapo ndipo Ujumbe ulipotangazwa kwanza. Hiyo ni kweli? "Toba na ondoleo la dhambi lihubiriwe katika Jina Lake, kuanzia Yerusalemu."

Sasa, kwanza, tutafanya kama Yeye alivyofanya: kuwa na maombi ya kuwaponya wagonjwa.

Halafu, tutakuwa na karama kuu: Maji yako tayari, hapa nyuma, kwa yeyote anayetaka kubatizwa (kuna nguo hapa kwa ajili ya wanawake, mavazi humu ndani kwa ajili ya wanaume), yakiwa tayari kwa ajili yenu kusamehewa dhambi zenu; kwa sababu kumbuka, ya kwamba unaweza tu kusamehewa dhambi zako kulingana na mafundisho ya Biblia. "Kwa maana hakuna Jina lingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu, ambapo huna budi kuokolewa kwalo."

Paulo alikutana na wengine ambao tayari walikuwa wamebatizwa. Nao walikuwa wakipiga makelele, walipata ushindi. Yeye alisema, "Mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

Wao walisema, "Kwa ubatizo Yohana."

Yeye alisema, "Yohana alibatiza kwa toba." Sasa, pata jambo hili: utubu, si kwa ondoleo la dhambi. Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo? Si kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Walibatizwa vema, wapate kutubu. Walikuwa wametubu: "Naam, bwana, nimetubu. Mimi, nikiamini Yeye yuaja." Walibatizwa katika toba; hiyo ni kusema, "kumwamini Bwana Yesu Kristo."

Ndipo waliposikia jambo hili (ya kwamba Dhabihu tayari imekuja), walibatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo. Na halafu, ikatolewa kwao, alipoweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu; nao wakanena kwa lugha na kutabiri.

Sasa, utabadilishaje Maandiko hayo? Weka kidole chako mahali pamoja katika Biblia ambapo mtu ye yote alipata kusamehewa dhambi zao, katika Agano Jipya, na aliyewahi kubatizwa kwa njia nyingine yo yote ila katika Jina la Yesu Kristo.

Nionyeshe mahali pamoja katika Biblia ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Ama nitaleta kwenye dawati langu historia, historia ya kanisa inayoonesha ambapo mtu ye yote alibatizwa katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, mpaka miaka mia tatu na kitu baada ya kifo cha mtume wa mwisho, wakati Kanisa Katoliki liliunda madhehebu.

Sasa, ninao Baba wa Kabla ya Nikea, na … wanahistoria wote, na kila kitu, moja kwa moja katika utafiti wangu: historia ya kale sana, takatifu ulimwenguni; thibitisho pekee tulilo nalo lisilokosea.

Someni *Our Sunday Visitor*, ama katekismo ya kanisa Katoliki, na uwaangalie, yale wasemayo: "Huenda baadhi ya Waprotestanti wataokolewa, kwa sababu wanainamia fundisho la Katoliki: Kwa kuwa Biblia yao inasema, 'kubatiza katika Jina la Yesu Kristo, "bali tumeondoa heshima kwenye 'Jina la Yesu,' na kuiweka juu ya 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,' nao wanalikubali."

Sasa, nionyeshe Andiko kinyume na hilo.

Na hivyo ndivyo ilivyo. Na hata hivyo, ulimwengu unauinamia. Kwa nini? Hawajawahi kufika Kalvari. Hivyo ndivyo ilivyo. Hawajawahi kuona.

Watakudhihaki na kukuita … hata watakuita, "Mtakatifu anayejiviringisha," "Yesu pekee," na majina hayo yote ya ushupavu wa dini wanayoweza. Inaleta tofauti gani kile wanachokuita? Walifanya nini … Yeye alijali walivyomwita? Alisulubishwa. Yeye aliishi kwa ajili ya Mungu, na Mungu peke yake. Na kama Roho yule yule, aliyekuwa ndani Yake, yumo ndani yako, atakufanya ufanye jambo lile lile: ukichukua Jina Lake. "Lolote mfanyalo" (inasema Biblia) "kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Yesu, mkimtukuza Mungu."

Unapata wapi huo utatu, fundisho la kipagani? Kutoka kwenye katekisimo, si kutoka katika Biblia. Neno "utatu" hata halijatajwa katika Maandiko yote kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Hakuna kitu kama hicho. Hakuna kitu kama mungu wa utatu. Yeye ni Mungu, Mungu pekee, Mungu mmoja. Daima imekuwa ni Mungu mmoja. Alitumikia ofisi tatu: Yeye aliwahi kuwa Baba, chini ya Musa. Alitumikia mara moja katika mwili, kama Mwana, Yesu. Yeye anatumikia sasa kama Roho Mtakatifu. Lakini ni Mungu mmoja. Mungu mmoja, si mwenye majina matatu. Ofisi tatu, vyeo vitatu katika Jina moja: Yesu Kristo.

Cho chote tofauti ni cha kipagani; nami naomba mtu fulani aoneshe jambo hilo, kama sivyo. Hiyo ni kweli. Nimesema jambo hilo kwa miaka baada ya miaka baada ya miaka, na hakuna mtu aliyechukua jambo hilo, bado (mnaona?), kwa sababu haliwezi kuwa. Nina ninii … hii hapa Biblia, kwanza; na kuna zile historia za kale kuthibitisha ya kwamba ni kweli kabisa. Na kwa nini Ibilisi ana …? Mimi … Vema, Biblia ilisema wangekuwa namna hiyo: "Wanawezaje kuja, nisipowavuta?" Hilo tu ndilo ninalolijua. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema, kwa hiyo …

Sisemi hilo kuwa … Kama ningalisema hivyo, na kuhubiri mahubiri kama haya, ningekuwa mnafiki wa hali ya chini sana miongoni mwenu. Hiyo ni kweli. Ninasema hivyo kwa sababu ni Kweli na ni Uzima. Wote waliobatizwa katika Kristo, wanamvaa Kristo. Wana Uzima, kwa Jina Lake.

Tunaomba katika Jina Lake, kutafuta katika Jina Lake, kuhubiri katika Jina Lake, kubatiza katika Jina Lake, kuishi katika Jina Lake, kufa katika Jina Lake, kwenda Mbinguni katika Jina Lake, kufufuka katika Jina Lake. "Jamaa yote ya Mbinguni inaitwa Yesu." Biblia ilisema hivyo: "Jamaa yote duniani inaitwa Yesu." Yeye alisema, "Nilikuja katika …"

Unasema, "Vema, ni Jina la Baba."

*Baba* si jina, ni cheo. Yeye alisema, "Nilikuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea." Sasa, Yeye alikuja katika Jina gani? A-ha. Hakika, " … wala hamkunipokea."

Kwa hiyo ndivyo ilivyo; ni haki, naam, imefichwa machoni pa wenye hekima na akili. Hakika, hakika ni kwamba, a-ha.

Na katika Ufunuo, kama tulivyofundisha hivi majuzi: kuna lile kanisa la kale la kahaba, ambalo ndilo dhehebu la kwanza; na halafu alikuwa na kundi la binti ambao walizaliwa kwake. Wanafanya jambo lile lile, tabia ile ile. Yote yanaishia Babeli, vivyo hivyo, pamoja na … pamoja na kanisa la Rumi na muungano wa makanisa ya—ya mataifa; na huyo hapo, wote wakiishia, wote katika kitu kile kile, mashua ile ile.

Lakini Kanisa la Mungu (Haleluya!), Ni Kanisa lililoitwa, lililotengwa. Kanisa limejengwaje? Utajuaje jambo hili? Unawezaje kujua jambo hili kuwa ni Kweli? Mungu anapokufunulia. Habili alijuaje—Habili alijuaje alikuwa mwana-kondoo badala ya matofaa? Ilifunuliwa kwake: "Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi."

Akishuka kutoka kwenye Mlima wa Kugeuzwa, Yesu anasema, "Watu husema mimi ni nani?"

Wengine walisema, "Eliya," "Musa," na kadhalika.

Yeye alisema, "Lakini ninawauliza, 'Mnasema mimi ni nani?'"

Petro alisema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

Yeye alisema, "Hukujifunza hili …" Kwa vinginevyo (nasema hivi, si kuwa mkubwa, bali kusisitiza jambo fulani): "Hukujifunza jambo hili katika seminari fulani; mtu fulani kamwe hakukufundisha jambo hili; bali Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia hili: ya kwamba MIMI NIKO (si Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, bali, Mimi ni Yesu Kristo). Na juu ya mwamba huu (Ni mwamba gani? Ule ambao Habili aliundea; juu ya mwamba ule ule.), Juu ya mwamba huu, Ukweli wa kiroho uliofunuliwa wa Mungu, nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu kamwe haitalishinda." Hiyo ni kweli. Wanajaribu, bali hawatashinda kamwe. Mnaona?

Kwa hiyo nenda tu Kalvari, ukasulubiwe, urudi, na uchukue njia yako pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, songa mbele.

Sasa, Bwana, tunakukabidhi mambo yote. Sijui, kutoka kwenye kundi hili, kuna nini hapa. Sina wazo la kujua, Bwana, isipokuwa Wewe ulifunue. Na sasa, Baba Mungu, sikuombi Wewe ufanye hivyo. Nimeliweka tu kwenye mapaja ya watu. Hao hapo. Jalia hii iwe Kalvari halisi asubuhi ya leo; jalia iwe ni kusulubiwa halisi kwa mapenzi ya nafsi, na kwa tamaa za kibinafsi, na kwa mambo makuu ya maisha.

Jalia watu wawe wanyenyekevu, na wawe tayari kuchukua njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Jalia watembee kwa unyenyekevu. Jalia wazaliwe katika Ufalme huu, Ufalme huu mkuu wa Mungu, ambao ni mwili wa kiroho, mwili wa kimbinguni wa Kristo duniani: "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa mwili mmoja."

Tujalie, Bwana. Kama ni weusi, weupe, manjano, kahawia, cho chote kile, mwanamume ama mwanamke, mtumwa au huru: sote tumenyweshwa Roho yule yule.

Tujalie, Baba, na iwe pamoja na … miongoni mwa wengi, asubuhi ya leo, wapate kufahamu; jalia ufungue ufahamu wao. Halafu, itakuwa kama siku mpya kwao: jua litawaka, na nuru mbaya ya theolojia za kujibunia zitatoweka, na Nuru ya Mungu itaangaza njiani mwao, na kupasua pazia lililo ndani ya pazia Nuru hii nzuri. Nao wanaweza kutembea kwenye barabara kuu ya utakatifu, basi, wakiishi kwa ajili ya wengine, kama Kristo alivyofanya.

Sasa tunapoingiza mstari wa maombi, ninaomba ya kwamba utawatia mafuta watumishi Wako asubuhi ya leo, sisi sote, tunapoomba, mmoja kwa mwingine. Na jalia, leo, kwamba kila mtu mgonjwa anayepitia kwenye mstari huu wa maombi apate kuponywa. Jalia warudi, kama yule msichana mdogo mwenye makengeza, na yule mvulana mdogo, na yule … na yule mama mzee, na—na Ndugu Wright, na wengi wa wale waliopitia, Bwana, wakiwa na mateso na magonjwa na kitu fulani ambacho madaktari wasingeweza kuponya; na hawa hapa leo (kama tu juma moja lililopita), na hawa hapa, vema, leo.

Mungu, jalia wanaume na wanawake wapitie kwa imani ile ile, wakijua ya kwamba wanaenda Kalvari kusulubiwa kwa mawazo yao na maoni yao ya kwamba "wamepita uponyaji." Jalia nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini zipe uhai, maisha makuu ya imani.

Halafu basi, mara baada ya jambo hili, naomba wengi waje kwenye kidimbwi kwa ajili ya ubatizo. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, tuna dakika ishirini tu kuendesha mstari wa maombi na ibada ya ubatizo. Sasa hatuna kadi za maombi. Tumetoka kwenye jambo hilo, nasi tutajaribu kulifanyia kazi katika mikutano yangu mikubwa kila tunapoanza. Nimewaambia ninyi nyote, tuliuweka, tuliuweka kwenye kanda, na popote niendako, hizo kanda zitatumwa kabla.

Ishara inaelekeza tu kwenye baraka. Wazo lilikuwa, "Kama utawaombea wagonjwa, wafanye watu wakuamini."

Nikasema, "Hawangeniamini."

Yeye alisema, "Utapewa ishara hizi, na kwa hili wataamini." Ishara zimeendelea na kurudiarudia, kwa miaka kumi kote ulimwenguni, bila hata wakati mmoja kushindwa. Hakuna kushindwa, hata kidogo, ndani yake. Ni wangapi wanaojua jambo hilo kuwa ni kweli?

Vema, kama unaweza kuamini ishara, basi amini Ujumbe. Hiyo ni kweli. Inaonesha jambo hilo. Na je! Mungu angeweka ndani yangu Ujumbe (Na hebu uwe mkamilifu sana namna hiyo, lakini nini …) nami nawaambia jambo fulani lingekuwa la uongo? Mungu hataniruhusu nifanye hivyo. La, la. La, bwana. Ninawaambia Kweli.

Sasa, ninyi nyote mnaotaka kuombewa, kwa namna fulani, kwenye safu hii hapa, njoni upande huu, mkiweza, kule, fanyeni mstari upande wa kulia. Na basi hilo litawafanya watu waje moja kwa moja kadri tunavyoomba. Ndipo tutawapata wa—wavulana, mabawabu na wengineo wataangalia; na kadri wanavyopitia hapa, kisha upande huu, tutawaleta kupitia upande wa nyuma, na kuwapitisha. Kila mtu aombewe.

[Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Loo, la, aha, mimi sikufanya hivyo. Vema, wakati wo wote unapotaka. Haijalishi. Unaweza kumtoa, ama wewe … Ninaweza … mlete huko nje sasa, ama baadaye kidogo, wakati wo wote atakao, haidhuru.

Sasa, hebu na tunyamaze tuwezavyo, kwa dakika chache zijazo. Ninawatakeni ninyi nyote mfikirie sasa: Sasa, Biblia ilisema nini—nini? "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa." Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya"? Na kazi zilikuwa ni nini? Yeye alisema, "Ninaweza kama mnaamini ya kwamba ninaweza kufanya jambo hili." Hiyo ni kweli?

Swali langu lilikuwa nini? "Hawataniniamini."

Yeye alisema, "Ishara hizi zitawafanya waamini."

Sasa, kama unaamini, jitayarishe: Hii ndiyo saa yako ya ukombozi. Ni kama tu vile itakavyokuwa kutokana na dhambi, ni ahadi ile ile ya Mungu yule yule.

Sasa, tuna maskini, mwanamke mgonjwa hapa, aliye na ugonjwa wa tumbo, kutoka huko New Albany. Tutamwombea, kwanza, ili aweze kumpatia ninii yake—kumpatia kiti. Sasa, kwa utulivu, na kila mtu, sasa. Ninataka ndugu wanisaidie, hapa. Na hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, sasa, kwa ajili ya maombi.

Sasa, Baba wa Mbinguni, hili limekuwa ni Neno Lako. Mimi sihusiki na hatua ambayo itachukuliwa juu yake, bali ninawajibika kwa kulihubiri. Na kujua jambo hili (na kujua ya kwamba mimi ni mtu wa makamu sasa, na siku moja sina budi kukukabili Wewe): nimehubiri Kweli kutoka moyoni mwangu. Unajua jambo hilo. Si kuwa na upendeleo, kama hivyo ndivyo ilivyokuwa, Bwana, basi ninahitaji toba.

Na Baba, ninaomba ya kwamba utasaidia, sasa, tunapoenda kuwaombea wagonjwa, jalia maombi yangu yajibiwe, si maombi yangu tu, Bwana, bali maombi ya kanisa hili, kama watu hawa maskini … Vipi kama huyu alikuwa ni mke wangu anayesimama hapa? Vipi kama huyu alikuwa ndiye, ameketi kwenye kiti cha magurudumu? Au dada yangu? Mama yangu? Loo, Mungu, waponye watu hawa. Utafanya hivyo, Bwana?

Angalia, wakisimama kwenye mstari wa maombi: ugonjwa wa moyo, saratani, uvimbe, kila namna ya magonjwa na mateso. Wengi wao wanakuja (mamia wanaokolewa, moja kwa moja kutoka hapa, Bwana), nao wanaona jambo hilo, nao wanaamini, nao wanakuja kwenye mstari wa maombi kukubali wao. Wanakuja kwenye Jiwe lililo hai sasa, si mtumishi Wako, bali kwa Mwanao, Yesu, Ambaye ni Kiongozi wa Kanisa, Mtu wa kiroho, wa siri miongoni mwetu. Na tunapoenda, tukilitoa Jina Lake (Wewe ulisema, "Katika Jina Langu watatoa pepo."), ninaomba ya kwamba utajibu maombi yetu, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, kila mtu awe katika maombi. Sasa, hii ni sehemu yako, pia. Haya ndiyo maombi yako.

Sasa maskini mwanamke huyu hana budi kufa, kama kitu Fulani hakimsaidii.

Ni wangapi wanaomjua Ndugu Stadsklev? Ndugu na Dada Stadsklev? Niliitwa kutoka Ujerumani mara tatu usiku ule mwingine; mtoto wao mchanga alikuwa amekufa. Waliuliza, "Ndugu Branham, tumekuona, kwa Roho wa Mungu, ukiwafufua wafu," (Walisimama sasa na kuangalia jambo hilo. Unaona?) "Nasi tunajua ya kwamba wewe ni nabii wa Bwana. Sema tu Neno."

Nikasema, "Siwezi kulisema, isipokuwa liwekwe kinywani mwangu."

"Njoo Ujerumani." Niliamka upesi sana. Nao wakanipigia simu: "Tumepata ndege ambayo inaweza kukuleta Ujerumani katika masaa sita." Ndege ya jeshi ambayo ingeniendesha kwenda Ujerumani kumfufua mtoto aliyekufa. Ndege ya jeshi ingenipeleka ndani ya saa sita, kutoka Louisville hadi Munchen, Ujerumani.

Niliingia mle, na kupiga magoti, na nikasema, "Baba, niseme nini? Nena kinywani mwangu." Yeye hakunijibu. Nilitoka nikaenda mwituni, nikasema, "Baba, niseme nini? Weka maneno kinywani mwangu. Nitaenda bure, kama sivyo." Nikarudi, Yeye hakunijibu. Nikaingia ndani. Usiku kucha niliomba, "Bwana, weka maneno hayo kinywani mwangu." Hakuna kitu kilichojibiwa.

Kesho yake asubuhi mke wangu aliamka. Mara tu alipoondoka, Neno (nikasimama), Yeye alisema, "Usikemee jambo hili. Huu ni mkono wa Bwana." A-ha.

Kisha upesi nikaenda kwenye simu: "Siwezi kuja. La, huu ni mkono wa Bwana. Nimekatazwa." Mnaona kuna nguvu gani juu ya kemeo hilo? Wakati Mungu aliposema, "Usifanye hivyo, kwa kuwa ni mkono wa Bwana."

Sasa, Musa, wakati mmoja, aliambiwa asifanye jambo fulani, akaenda na kulifanya hata hivyo. Mnakumbuka? Kwa hiyo si—sikwenda.

Nami ningeweza kuwaletea taarifa za kuwaonesha watu wanne mbalimbali, ambao, walitangazwa wafu na madaktari, baada ya maombi na kukemea mauti. Mnaona? Tunasimama mle ndani kukemea jambo hilo. Na kama Mungu alikupa nguvu za kufanya jambo fulani, afadhali uwe mwangalifu kwa yale unayofanya. Mnaona? Afadhali ujali … Yeye alisema, "Usininii …"

Sasa, kumbukeni, hilo huenda lisijipambanue kwako sana, bali kwangu mimi, lilimaanisha kitu fulani. Mnaona?

"Usikemee jambo hili." Sauti tamu sana, yenye fadhili (yapata saa kumi na mbili na nusu, ninaamini ilikuwa hivyo, saa kumi na mbili na nusu asubuhi hiyo) ilisema, "Usikemee jambo hili. Huu ni mkono wa Bwana."

Nikasema, "Asante, Baba. Asante, Bwana. Sitafanya hivyo."

Kama angalisema, "Kemea hili. Huyu ndiye adui aliyeingia kisiri."

Ningesema, "Hebu twende." Na lingefanywa.

Wakati mvulana huyo mdogo kule Finland alipokuwa amelala pale, amekufa, amepondwa, hakuna hata mfupa mzima katika mwili wake, Bwana alisema, "Huo ulikuwa ni mkono wa Shetani," kasema, "ukemee."

Nami nikasema, “Mauti, huwezi kumshikilia. Mrudishe, mwachilie.” Hapo, akaruka kwa miguu yake, vema, bila hata mfupa uliovunjika mwilini mwake. Hilo ni Neno la Bwana. Siwezi kutumia Neno la Bwana mpaka Neno la Bwana litakaponijia.

Lakini katika Maandiko, Neno la Bwana limenipa agizo la kuwaombea wagonjwa hawa; nikupe agizo la kuwaombea. Sasa, “maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa;” hebu na tuombe, inueni vichwa vyenu; tutaona yale anayosema, unapopita.

Wewe ni Mkristo, sivyo? Unaamini kwa moyo wako wote kwamba Yesu atakuponya? Una shida kidogo ya tumbo; umeugua kwa miaka mingi, dada. Sasa, utapona, kama utaamini.

Sasa, Bwana Mungu, mwanamke huyu kijana hana budi kufa isipokuwa Wewe umsaidie. Sasa ninaomba, ninapomtazama, sioni sababu ya yeye kufa.

Nami ninajisikia katika roho yangu, Bwana, ya kwamba ni mapenzi Yako yaliyoruhusiwa, sasa, ya kwamba ninamkemea huyu: Shetani, mfungue!

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia apate afya, aje kwenye kanisa hili, na atoe ushuhuda kwa utukufu wa Mungu. Amina.

Sasa, kwa urahisi kama huo, mama, utapona. Unaamini ndugu hapo?

[Ndugu Branham anaondoka kwenye maikrofoni — Mh.] Je! Unaamini hapa chini, ya kwamba utakuwa mzima?

Nenda sasa, anza kula cho chote u … utafkachoweza basi, itakuwa sawa.

Sasa, unatarajia kuupa ulimwengu pigo, na kuupooza; ilikupiga, na kukupooza. Sasa, Mungu wa Mbinguni anayeondoa pigo Lake ulimwenguni ili kutoa ondoleo la dhambi, kwa Jina lile lile, anaweza kukupa ondoleo la dhambi, kukuondolea pigo, na kukufanya mzima afya.

Je! unaamini Yeye anaweza kufanya moyo huo udunde vyema? Ukifanya hivyo, utakuwa mzima …?

Bwana Yesu, maskini mwanamke huyu hana budi kukaa kwenye kiti hiki maishani mwake mwote na kisha, aondolewe. Lakini tunaomba ya kwamba nguvu hizi za Shetani ziondolewe kwake. Jalia aishi na atembee na awe wa kawaida kama alivyowahi kuwa. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Unaamini? Ni kazi iliyomalizika, imekwisha. Kuna nini? Bila hofu, bila … Si ninii …? Uliponywa saratani wakati mmoja …?… Fungukeni, mpeni Yesu kila kitu.

Bwana Yesu, ninaweka mkono wangu juu ya mwanamke huyu na kukemea ugonjwa wake. Ninajua yeye ni Mkristo, aliyezaliwa kwa Roho. Ninauondoa kwake, katika Jina la ajabu la Yesu Kristo. Amina.

Bwana Mungu, kwa ajili ya ndugu yake wa thamani, ninaomba wokovu wake katika Jina la Yesu. Simama juu ya jambo hilo. Amina. Litatendeka.

Je! Uko tayari kupokea uponyaji wako, mwanangu? Sawa, umeenda kwenye mkono Wake.

Bwana Yesu, juu ya kijana huyu, ambaye alisema, kutoka Kwako, anaomba apate uponyaji wake. Kama mtumishi Wako, ninaweka mikono yangu juu yake katika Jina la Yesu Kristo …?… Amina.

Sasa, ninii tu yo yote … sasa, wewe liitie tu Jina Lake. Sasa, si—si kwangu mimi …?…

Baba Mungu, kama mwana tu ambaye wakati mmoja aliegemea kifuani mwa mama yake, yeye amempapasa na—na akaomba pamoja naye na kuushika mkono wake mdogo alipokuwa mtoto aliyenong'ona. Sasa, Shetani amemweka katika kituo cha wagonjwa wa akili. Mungu, yeye amekuja kwenye Kanisa takatifu la Mungu aliye hai, Kanisa ambalo limezaliwa kwa Roho wa Mungu, Kanisa ambalo Roho wa Mungu anaishi ndani yake, na anajitambulisha Mwenyewe. Na leo, kwa maombi, tunamkomboa mwanamke huyo kutoka kwenye taasisi hiyo. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

Nenda nyumbani, uko sawa.

Asante kwa kuja, kuomba kwa ajili ya mama yako; huyo ni mwana halisi.

Hii ndiyo siku ya ukombozi wako. Bwana Yesu, kwa ajili ya mwanamke huyu kijana, kwa ajili ya wokovu wa mumewe na koo lake, jalia apokee katika Jina la Yesu Kristo, Ambaye anasema “njoo, amini sasa,” nalo ni tunda lililomalizika.

Bwana, madaktari wamesema, Bwana, iko mwilini mwake, ikiingia kwenye jicho lake. Amekuja kukombolewa, juu ya madhabahu hii, wakati Kanisa hili takatifu linapoomba, ninaomba ukombozi wake katika Jina la Yesu Kristo, janga hili litauacha mwili wake. Ni kazi iliyomalizika.

Kwa ajili ya mwanawe, ninabariki leso hii. Jalia kusikia na hali nzuri zirudie sikio lake …?

Sasa Kanisa linanena; sasa Kanisa ni Mwili wa kisiri wa Kristo. Sote tunakuombea. Mnaona? Hatu—hatukiri kuwa ulimwenguni tena. Hatuzungumzi juu ya kushangaa tuendako. Tulipata Njia. Tulizaliwa katika Njia hiyo. Sisi ni Kanisa la Mungu Aliye Hai (sehemu yake); bila shaka, limetawanyika kote ulimwenguni. Lakini hili ni kundi miongoni mwalo. Leo, pamoja tunakuja katika Jina Lake. Tunakuja kufanya yale aliyosema, tufanye. Ni kitu gani asichoweza kufunua tunapokutana. Waombee wagonjwa, wawekee mikono, "maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa."

Jalia ugonjwa wako wa moyo ukuache. Katika Jina la Yesu Kristo, ninatii agizo ambalo Mungu alinipa …?…

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7